epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatatu Julai 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581745
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 12
WACHEZAJI 6 WANAOWEZA KUTWAA BALLON D'OR 2024



# Dk. Mwigulu aibuka sakata la Tril. 1.7/-

• **Ni** zilizotolewa BoT, adai serikali... *Ukurasa 2*

**UKURASA WA 3**
**Uchunguzi** waanza vitambulisho NIDA kufutika maelezo



**UKURASA WA 5**
**NMB** yashinda tuzo 5 kimataifa, yatajwa benki bora Tanzania

**UKURASA WA 18**
**Kipindupindu** chaua, watu 105 walazwa katika kambi maalum



## Jamii yapewa hadhari kuhusu matumizi ya vijiti vya meno

UKURASA 4



Madaktari bingwa wa upasuaji kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), wakiendelea na upasuaji kwa mtoto Maliki Hashimu (5), mkazi wa Goba mkoani Dar es Salaam, aliyejeruhiwa koo na dada wa kazi Julai 15, mwaka huu. **PICHA: MNH**

# Ilivyo tiba mtoto aliyekatwa koromeo na msichana wa kazi

• **Samia** kulipa gharama Muhimbili... *Endelea ukurasa 5*

**MICHEZO** **KOCHA WA AUGSBURG AICHAMBUA YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Rais Hussein Ali Mwinyi akiungana na viongozi wa serikali, dini na wananchi katika Sala ya Maiti ya aliyekuwa mjane wa Sheikh Hyder Jabir Saleh E-Farsy, Zulekha Ahmed Abdallah, katika Msikiti Mkuu wa Ijumaa Malindi, Wilaya ya Mjini Unguja jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwigulu aibuka sakata la Tril. 1.7/-

**Na Mwandishi Wetu**

SAA chache baada ya gazeti Nipashe Jumapili kuripoti kuhusu lilichokiita utata wa Sh. trilioni 1.7 kutolewa katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Waziri wa Fedha Dk. Mwigulu Nchemba ameibuka na kutoa ufafanuzi kuhusu suala hilo.

Katika toleo lake la jana, gazeti hilo liliripoti kuwa Sh. trilioni 1.7 zilizotolewa BoT katika mwaka 2022/23 na kutumiwa na serikali ilhali hazikuwa sehemu ya makusanyo ya serikali kwa mwaka huo wa fedha.

Katika ufafanuzi wake kupitia mitandaoni ya kijamii jana, Waziri Mwigulu alisema serikali ilichukua fedha hizo BoT kama "advances or short term loans".

Alitaka wananchi wapuuze suala hilo ambalo jana liliteka mijadala ya mitandao ya kijamii, akisisitiza BoT inasimamia kwa umakini sheria za nchi na miiko ya benki kuu zote duniani.

"Nimesoma taarifa hiyo (ya Nipashe Jumapili) ambayo inatokana na uchambuzi wa NGO iitwayo WAJIBU inayoongozwa na Mzee Ludovic Utuoh, CAG mstaafu.

"Kwa ujumla, maelezo ya taarifa hiyo yanaeleweka na hayana utata wowote, hivyo sijui kwanini mwandishi wa Nipashe ameeleza kuwa kuna utata BoT.

"Taarifa imeelezea suala ambalo ni la kawaida na huwa linafanyika kila mwaka kutokana na Sheria ya BoT inayoruhusu kutoa advances or short term loans kwa serikali ili kukidhi mahitaji ya matumizi ambayo yanakuwa hayajapata mapato.

"Kwa mujibu wa kifungu cha 34 hadi 37 cha Sheria ya BoT, serikali inaruhusiwa kukopa hadi asilimia 18 ya makusanyo halisi ya ndani ya mwaka uliopita.

"Hili limekuwa linafanyika hivyo tangu BoT ianzishwe. BoT ni benki ya serikali, serikali huchukua 'advance' kwa mujibu wa sheria badala ya kukopa riba kubwa kutoka benki za biashara.

"Hivyo, kwa mwaka 2022/23, serikali ilikuwa inaweza kukopa BoT kiasi kinachofikia Sh. trilioni 4.5. Hivyo, taarifa ya kuwapo mkopo wa Sh. trilioni 1.7 ni suala ambalo liko ndani ya wigo unaokubalika kisheria.

"Kiasi hicho kilipofika mwisho wa mwaka kilijumuishwa kwenye 'Treasury Bonds' za mwaka husika ambazo zinaendelea kulipia riba kama sehemu ya mikopo ya ndani," alisema Dk. Mwigulu.

Aliendelea kueleza kuwa utaratibu huo ni wa kawaida na ufanyika kwa Benki Kuu za nchi nyingi duniani, pindi serikali inapohitaji fedha za kugharamia bajeti wakati bado inaendelea kujipanga na kukusanya mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali.

"Ndio maana hata IMF waliridhika kuwa BoT na serikali wamezingatia sheria na taratibu za kimataifa kama inavyotakiwa. Kutokana na uzingatiwaji sheria hizo, Bodi ya IMF waliridhia kutoa USD milioni 300 kwa mwaka 2023/24 na Benki ya Dunia waliridhia kutoa USD milioni 750 kwa mwaka 2023/24," alisema.

Waziri Mwigulu alisema taasisi hizo ziliridhia kutoa fedha hizo kwa kuzingatia Tathmini ya Pili ya Programu ya IMF iliyofanyika Desemba 2023 iliangalia masuala mbalimbali yakiwamo ya mapato, matumizi, madeni, uzingatiwaji Sheria ya BoT, ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, urari wa biashara, thamani ya Shilingi na usimamizi wa masoko ya fedha nchini.

Dk. Mwigulu aliahidi BoT itaandaa taarifa kwa umma na kutoa elimu, akisisitiza ni serikali kuchukua 'advance' ya Sh. trilioni 1.7 Benki Kuu "ni suala la kawaida".

Katika ripoti yake jana, gazeti Nipashe Jumapili liliripoti kuwa uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23 uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU umebaini kuwa mwaka huo wa fedha, serikali iliidhinishiwa na Bunge kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.48.

Hata hivyo, ukaguzi wa CAG kuhusu Hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka 2022/23, ulibaini serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.88, kukiwa na ziada ya Sh. bilioni 400.

Vilevile, makusanyo yaliyopelekwa Mfuko Mkuu ni Sh. trilioni 38.447. Sh. trilioni 3.433 hazikupita Mfuko Mkuu wa Serikali.

Uchambuzi ukabaini kuwa serikali licha ya kukusanya trilioni 38.447 zilizopita Mfuko Mkuu, BoT iliipa (serikali) Sh. trilioni 40.18, hivyo Benki Kuu kuipa serikali Sh. trilioni 1.7 za ziada, zilizozua utata, hadi jana Waziri Mwigulu alipofafanua kuwa "serikali ilikopeshwa fedha hizo na BoT".

Vilevile, uchambuzi umebaini kuwa kati ya Sh. trilioni 3.433 ambazo hazikupita Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka huo wa fedha, Sh. trilioni 3.197 zilipelekwa moja kwa moja kwenye miradi.

**RIPOTI YA CAG**

Inaporejewa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23 kuhusu suala hilo, inaonesha kuwa katika mwaka huo wa fedha, serikali ilikusanya Sh. trilioni 41.880 ikiwa ni zaidi ya bajeti ya Sh. trilioni 41.480 kwa Sh. bilioni 400.

CAG anafafanua kuwa kati ya Sh. trilioni 41.880 zilizokusanywa, Sh. trilioni 38.447 zilipokewa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, hivyo kuwapo tofauti ya Sh. trilioni 3.4334.

CAG anasema tofauti hiyo inatokana na Sh. trilioni 3.656 zilizopelekwa moja kwa moja kwenye miradi kutoka kwa wadau wa maendeleo na makusanyo yaliyopelekwa Zanzibar ambayo hayapitii Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali pamoja na Sh. bilioni 223 zinazotokana na bakaa za makusanyo ya kodi za mwaka uliopita na makusanyo mengine yaliyopokewa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali nje ya makisio ya bajeti.

"Jumla ya matumizi yaliyofanywa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ili kugharamia matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23 yalikuwa Sh. trilioni 39.523 bila kujumuisha Sh. bilioni 665.80 zilizotolewa kama fedha zilizorejeshwa (refunds) na matumizi mengine kwenye jumla ya makusanyo ya Sh. trilioni 38.447, hivyo kusababisha nakisi katika Benki Kuu (BoT) ya Sh. trilioni 1.742 kufikia tarehe 30 Juni 2023," CAG anaeleza katika Ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu.

# Naibu Waziri ajiuzulu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, amemwandikia Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson barua ya kujiuzulu ubunge.

Kwa barua hiyo ya tarehe 21 Julai mwaka huu, ina maana kwamba Balozi Mbarouk pia amejiuzulu nafasi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge, Mbarouk ambaye ni Mbunge wa Kuteuliwa na Rais, amefikia uamuzi huo kutokana na changamoto za kijamii.

"Kwa mujibu wa barua aliyomwandikia Spika, Mheshimiwa Mbarouk amesema amefikia uamuzi huo kufuatia changamoto za kijamii zinazomkabili kwa sasa," sehemu ya taarifa hiyo ya Bunge inasomeka.

Uongozi wa Bunge unanukuu sehemu ya barua ya Balozi Mbarouk, akisema, "Ninalazimika kuchukua uamuzi wa kujiuzulu ili nipate nafasi ya kushughulikia changamoto hizo."

Machi 31, 2021, Rais Samia alifanya uteuzi wa wabunge watatu na kufanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri, Balozi Mbarouk akiwa mmoja wa wateule hao.

Balozi Mbarouk amewahi kuwa Balozi wa Tanzania katika Jamhuri ya Kiislam ya Iran, pia Balozi wa Tanzania Pakstan na Bahrain kuanzia Mei 27, 2013 hadi Novemba 2019.

## HABARI KITAIFA

# Uchunguzi vitambulisho NIDA kufutika maelezo waanza

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inafanya uchunguzi kubaini kilichosababisha kufutika baadhi ya maelezo muhimu kwenye vitambulisho vya taifa 21,224 vilivyotolewa hivi karibuni na kusambazwa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Vitambulisho, Edson Guyaye, alisema mamlaka inachunguza ikiwa tatizo hilo limetokana na hitilafu za mashine za uzalishaji, wino au kadi ghafi ili kulitatua bila gharama zaidi.

"Tunaasa wananchi kuchukua hatua wanapokutana na vitambulisho vya namna hii. Mtu yeyote ambaye kitambulisho chake kina kasoro kama hizo anapaswa kukirudisha kwenye kituo cha kukusanyia au ofisi ya NIDA iliyopo karibu naye," alisema Guyaye.

Alisema mamlaka inatambua kuna kadi 21,224 zenye kasoro, ikiwa ni pamoja na kufutika majina, picha na tarehe za kuzaliwa. Kadi hizo ni sawa na asilimia 0.09 ya vitambulisho vya taifa 21,322,098 vilivyotolewa.

Alibainisha kuwa serikali ilitenga Sh. bilioni 42.5 kwa ajili ya kununua kadi za ghafi Oktoba mwaka jana.

Alisema lengo lilikuwa ni kuboresha uzalishaji wa vitambulisho, usambazaji na utoaji kadi za kitambulisho cha taifa pamoja na kukidhi mahitaji ya umma.

Guyaye alisema mchakato huo ulilenga zaidi kutoa kadi za vitambulisho kwa raia wote wenye namba ya utambulisho (NIN) kwa kuzisambaza kupitia mamlaka za serikali za mitaa na ofisi za NIDA nchini.

Guyaye pia alithibitisha kuwa takribani kadi milioni mbili, hasa katika maeneo ya mijini, hazijachukuliwa. "Kumekuwa na habari potofu kuhusu ubora wa kadi hizi. Zinakidhi viwango vyote vya kimataifa vinavyohitajika. Tatizo hili ni tukio dogo linaloweza kutokea katika viwanda vya uzalishaji."

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa NIDA, Geoffrey Tengeneza, alipozungumza na waandishi wa habari Aprili 27, mwaka huu, NIDA imesajili zaidi ya watu milioni 24 tangu kuanza mchakato wa usajili wa vitambulisho hivyo mwaka 2012, huku zaidi ya watu milioni 20 wakipatiwa namba ya utambulisho. Tengeneza alisema pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika mchakato huo, mamlaka imesajili asilimia 79 ya watu wenye umri wa kuanzia miaka 18.

"Hadi kufikia Februari, mwaka huu, NIDA imefanikiwa kusajili watu 24,495,804 ambao ni asilimia 79 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea katika watu 31,477,938 wenye sifa za kusajiliwa.

"Lakini pia tumefanikiwa kutoa namba za utambulisho wa taifa (NIN) kwa watu 20,832,225 ambao ni sawa na asilimia 85 ya watu waliotambuliwa na kusajiliwa. Mamlaka pia imezalisha vitambulisho 20,286,420 ambavyo ni asilimia 97.4 ya watu waliokuwa na namba ya utambulisho," alisema.

Hata hivyo, hivi karibuni NIDA ilieleza kuwa imebaini kuwapo idadi kubwa ya vitambulisho hivyo katika ofisi za serikali za mitaa, kata, vitongoji, vijiji, wilaya na mikoa kutokana na wahusika kutokwenda kuvichukua, huku mkoa wa Dar es Salaam ukitajwa kuongoza kutokana na wengi kutegemea kutumia namba walizopatiwa awali.

# Wadau walaani utekaji watoto

**Na Halfani Chusi**

WADAU wapenda haki za watoto wamelaani vitendo vya kutekwa, kuibwa na mauaji ya watoto, wakitaka serikali ichukue hatua za makusudi kupambana na matukio hayo.

Walitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam walipoomboleza na kuwaombea watoto walioripotiwa kutekwa na kuuawa nchini hivi karibuni.

Katika maombolezo yao, wadau hao walifanya ibada ya kuwaombea kisha wakawasha mishumaa kama ishara ya kukumbuka watoto hao.

Walikumbushia kuwa Juni 3, mwaka huu, mkoani Kagera, mtoto Asimwe Novart mwenye umri wa miaka miwili, alitekwa akiwa mikononi mwa mama yake na baadaye kukutwa amefariki dunia akiwa amenyofolewa baadhi ya viungo.

Julai 15 mkoani Dodoma, kuliripotiwa tukio la mtoto Sumaiya Issa kutekwa na mpaka sasa hajapatikana; Julai 7 mwaka huu, huko Mbagala Dar es Salaam, mtoto Nusra Omari alikutwa ameuawa na baadhi ya viungo kunyofolewa; Julai 17 mkoani Dodoma, mtoto Theresphoa Mwakalinga alikutwa amefariki dunia na baadhi ya viungo vyake vimenyofolewa. Mdau wa haki za watoto kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Getrude Dyabene, alisema anatambua jitihada zinazofanywa na serikali kulinda watoto, lakini wanasikitika kuona ukatili dhidi yao unaendelea.

Alisema vitendo hivyo si tu kinyume cha haki za binadamu, bali pia ni kinyume cha Katiba ya Tanzania na sheria za nchi.

"Jeshi la Polisi limekuwa likitolea taarifa matukio ya aina hiyo, hata hivyo haturidhishwi na mikakati iliyowekwa ya ufutiliaji ili kukomesha vitendo hivyo.

"Kwa hali ilivyo sasa tulitarajia Jeshi la Polisi lifuatilie kwa umakini zaidi kujua chanzo cha haya matukio na wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua stahiki," alisema Getrude.

Akiwasilisha hoja zao kwa serikali, akianza na Rais Samia Suluhu Hassan, mdau kutoka Shirika la Msichana Initiatives, Rebeca Gyumi, alisema "Rais kama Amiri Jeshi Mkuu, tunamwomba aendelee kusisitiza ulinzi na usalama wa mtoto.

"Taasisi zote zenye mamlaka ya ulinzi wa raia zitimize majukumu yake na kukamilisha kwa haraka uchunguzi wa kiini cha matukio haya na upelelezi kwa matukio yaliyotokea."

Mdau mwingine kutoka Mtandao wa Haki za Watoto, Msafiri Mwajuma, alishauri Jeshi la Polisi kufuatilia kwa haraka na kuweka kipaumbele tarifa za watoto kupotea pasipo kusubiri kupita saa 24.

"Wazazi, walezi, jamii, walimu kwa ujumla tuongeze ulinzi kwa watoto tuhamasishe watoto kutembea katika makundi tuunde vikundi vya ulinzi shirikishi katika jamii zetu na kuwaelimisha watoto wasikubali kuambatana na wasiowafahamu," alisema.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Jamii yatahadharishwa utumiaji 'toothpick'

**Na Christina Mwakangale**

BINGWA wa Upasuaji, Kinywa, Meno na Uso (Oral maxillofacial Surgeon), Dk. Gemma Berege, ameiasa jamii kuhudhuria kliniki walau mara moja kwa mwaka kwa watu wazima na kwa watoto mara mbili kwa kipindi hicho.

Pia ameishauri jamii kuepuka matumizi ya vijiti vya meno (toothpick), wanapohitaji kuondoa vipande vya chakula vilivyosalia katikati ya meno, kuepuka kusogeza meno na kuharibu msingi wake.

Alisema miongoni mwa tatizo kuu la kinywa ni asilimia 60 ya wanaochunguzwa kubainika meno kuoza na kutoboka, kutokana na ulaji wa vyakula vyenye sukari, kutotunza kinywa, magonjwa mbalimbali kama vile kupungukiwa mate.

Bingwa huyo aliyasema hayo katika mahojiano na gazeti hili, kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara Kimataifa Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba, yaliyohitimishwa Julai 13, mwaka huu na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Dk. Gemma alisema meno kuharibika ni hatari ya kuyapoteza na hasara za kupoteza meno ni; mfupa wa taya unaoshikilia meno kusinyaa; meno kusogea au kurefuka na kusababisha mng'atano.

Hasara nyingine ni; kubadilisha mwonekano wa sura; kushindwa kutamka, baadhi ya matamshi, maneno na kusababisha mzungumzaji kutofikisha ujumbe unaotakiwa ipasavyo kwa msikilizaji

"Kinywa tunapendekeza angalau kifanyiwe usafi kwa kuswaki mara mbili kwa siku, asubuhi na usiku. Hii inasaidia kuondoa mabaki ya vyakula yatakayozalisha bakteria, kisha meno kutoboka na kuoza," alisema Dk. Gemma:

"Matumizi ya 'toothpick' kama yalivyozoeleka kwenye jamii hatuyashauri. Vijiti hivi unapotumia mara kwa mara husababisha msingi wa meno ambao ni fizi kuharibika na meno kusogea, utaharibu taswira ya sura na mdomo."

Kadhalika, Dk. Gemma alizitaja faida za kufanya upandikizaji wa meno kama vile, kuzuia mfupa unaoshikika meno usisogee na kuwezesha kuweka meno ya bandia inapohitajika.

"Kipandikizi cha meno kina asili ya chuma halafu baada ya miezi sita utawekewa meno ya bandia. Huduma hii imeanza rasmi MNH mwaka jana Idara ya Meno. Upandikizaji unatumia dakika 20 na kama mfupa wa taya umepungua unavunwa mfupa katika kidevu," alisema.

"Jamii wasitenganishe mwili kwa kuzingatia kliniki ya ugonjwa mmoja tu, kama vile ya presha, mifupa, badala wapende kuchunguza mwili mzima. Utasikia mtu anasema nina kliniki ya moyo, kinywa je?"

Alisema watu wanaweza kujenga utaratibu wa kuchunguza afya ya kinywa, mara moja kwa mwaka katika kila wanapokumbuka siku zao za kuzaliwa.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kushoto), akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Nurdin Babu, kwenye Kijiji cha Mikungani wilayani Arumeru juzi, baada ya kutembelea miradi 57 yenye thamani ya Sh. bilioni 149.5. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wahukumiwa kifungo miaka 30 unyang'anyi wa kutumia silaha

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imewahukumu watu wawili kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kukutwa na kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Waliohukumiwa ni Magabe Joseph (22) na Maneno Joseph (24), wote wakazi wa Mtaa wa Mwabasabi, wilayani Geita.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha mashtaka yote sita pasi na kuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao, ili iwe fundisho kwao na kwa vijana wengine wenye tabia ya wizi kama yao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Mussa Mlawa, ulipeleka mahakamani mashahidi watano na vielelezo vinne ambavyo vilithibitisha washtakiwa hao walitenda makosa hayo.

Hakimu huyo alisema washtakiwa wote wawili wametiwa hatiani kwa makosa yote sita, akawapa nafasi ya kufanya maombolezo ili mahakama iwapunguzie adhabu.

Washtakiwa wote kwa pamoja walitoa maombolezo ya kupunguziwa adhabu na kusema wana familia zinawategemea, pia wanaowazazi wanaowategemea.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Mussa Mlawa, uliomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Maweda alisema: "Mahakama hii inawahukumu washtakiwa wote wawili kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na mkimaliza kifungo chenu mtakuwa mmejifunza na kuwa raia wema. Rufani ipo wazi kwa upande wowote ambao haujaridhika na hukumu hii."

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mlawa alidai kosa la kwanza lilifanywa Desemba 29, 2022 katika Mtaa wa Nshinde, mkoani Geita kwa washtakiwa kwa pamoja kuiba simu mbili aina ya Itel zenye thamani ya Sh. 75,000 na 95,000.

Pia walidaiwa kuiba nguo mbalimbali na kufanya jumla ya mali za Sh. 170,000, mali ya Happiness Mtaswala. Ilidaiwa kuwa kabla ya wizi huo, washtakiwa hao walitumia mapanga kumtishia mlalamikaji ili kujipatia mali hizo.

Mlawa alidai kuwa kosa la pili lilifanywa Desemba 29, 2022 katika Mtaa wa Nshinde, mkoani Geita washtakiwa wote kwa pamoja waliiba sweta la mwanafunzi wa shule lenye thamani ya Sh. 12,000, fulana ya shule yenye thamani ya Sh. 12,000, simu mbili za mkononi; Tecno yenye thamani ya Sh. 300,000 na nyingine yenye thamani ya Sh. 45,000, kufanya jumla ya vitu vyote kuwa Sh. 369,000, mali ya Jona Misungwi.

Alidai kuwa kabla au baada ya wizi huo, washtakiwa hao walimpiga kwa ubapa wa mapanga kumtishia mlalamikaji ili kujipatia mali hizo.

Katika shtaka lingine, washtakiwa wote kwa pamoja walidaiwa kuiba Sh. 15,000 kutoka kwa Alphonce Kliyandukwa na kabla ya wizi huo washtakiwa walimtishia mlalamikaji kwa mapanga ili kujipatia fedha hizo.

Alidai kuwa katika shtaka la nne ambalo kosa lake linadaiwa kutendwa Desemba 29, 2022 katika Mtaa wa Nshinde, mkoani Geita, washtakiwa wote kwa pamoja waliiba betri ya sola aina ya Sunda yenye thamani ya Sh. 60,000, redio moja aina ya Aboda yenye thamani ya Sh. 15,000, simu mbili aina ya Itel zenye thamani ya Sh. 45,000 na fedha Sh. 60,000 na jumla ya vitu vyote vina thamani ya Sh. 275,000, mali ya Abasi Issa.Katika shtaka la tano, ilidaiwa kuwa Desemba 29, 2022, katika mtaa huo, washtakiwa wote kwa pamoja waliiba godoro lenye thamani ya Sh. 280,000, Tv moja yenye thamani Sh. 300,000 na simu moja aina Tecno yenye thamani ya Sh. 40,000.

Vingine walivyodaiwa kunyang'anya ni mashuka mawili yenye thamani ya Sh. 36,000, pazia moja lenye thamani ya Sh. 10,000 na viatu pea moja vyenye thamani ya Sh. 24,000, mali ya Fredi Jafeti. Kabla ya wizi huo washtakiwa wanadaiwa walimtishia mlalamikaji kwa mapanga ili kujipatia mali hizo.

Wakili Mlawa alidai mahakamani kuwa kosa la sita lilifanywa Desemba 29, 2022 katika mtaa huo, washtakiwa wote kwa pamoja wakidaiwa kuiba Sh. 7,000, mali ya Kulwa Kulyaudukwa, kabla ya wizi huo washtakiwa walimtishia mlalamikaji kwa mapanga ili kujipatia mali hizo.




# NMB yashinda tuzo 5 za kimataifa, yatajwa benki bora Tanzania 2024

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imenyakua tuzo tatu za ufanisi za kimataifa kutokana na mchango mkubwa wa huduma zake za kifedha katika kuboresha maisha ya Watanzania na kuchangia juhudi za ujenzi wa taifa.

Tuzo hizo za ubora za jarida la Euromoney ni mwendelezo wa kutambuliwa kwake ndani na nje ya nchi kwa umahiri na ubunifu ambapo mwaka jana ilishinda zaidi ya tuzo 30.

Ushindi wa NMB katika Tuzo za Ubora za Euromoney 2024 ni pamoja na kutunukiwa zawadi ya Benki Bora Tanzania kwa mara ya 11 katika kipindi cha miaka 12, ikiwamo mwaka 2023.

Jarida hilo kiongozi la masuala ya kifedha na mitaji duniani pia limeitunuku benki hiyo tuzo mbili mpya, ambazo ni Benki Bora ya Kidijiti Tanzania, Benki Bora kwa ESG inayohusiana na mambo ya mazingira, jamii na utawala bora na pia tuzo za Benki Bora ya Wateja Maalum na Wateja Wenye Mali.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo jijini London, Uingereza, Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali, Alfred Shao, alisema NMB imenyakua tuzo hizo kutokana na ubora wa masuluhisho yake bunifu ya kifedha na mchango wake wa kipekee katika ukuaji uchumi wa taifa.

"NMB inaamini katika utoaji huduma za kifedha ambazo zinapatikana kirahisi muda wote na wakati wowote. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa kwa ufanisi mkubwa, tunaendelea kuvumbua mifumo ya mtandaoni na ya kidijitali ili kumfikia kila mteja na kukidhi mahitaji yake ya huduma za kifedha," Shao alisema.

Tuzo za ubora za Euromoney zilianzishwa miaka 30 iliyopita, kutambua mafanikio ya benki na wataalamu wa tasnia hiyo kote ulimwenguni.

Mwaka huu, benki 600 kutoka nchi 100 zilishiriki tuzo hizo na kuzifanya kuwa moja ya programu kubwa ya kutambua ubora katika tasnia hiyo.

NMB ilitajwa kuwa Benki Bora kwa ESG nchini kutokana na umahiri wake wa uendelevu katika masuala ya fedha na dhamira yake ya kujitolea kuboresha maisha katika jamii inazozihudumia. Kwa mujibu wa Shao, kutambuliwa huko kunatokana na benki hiyo kuzingatia huduma endelevu za kifedha kama msingi wa mkakati wake ili kuhakikisha inatoa ushauri wenye tija kwa jamii, ufadhili na suluhisho za uwekezaji.

"Tuzo hizi tano si tu ni kielelezo cha mafanikio yetu bali pia ni motisha kwa ajili ya kuimarika zaidi siku zijazo. Tumejizatiti kuendelea kudumisha viwango vya juu vya ubora, uadilifu na huduma. Tutaendelea kuvumbua na kubadilika ili kukidhi mahitaji ya wateja wetu na sekta ya fedha kwa ujumla.

"Iwe ni kupitia programu za uelimishaji masuala ya kifedha, kusaidia biashara ndogo au kuendeleza utofauti na ushirikishwaji wafanyakazi wetu, tunajitahidi kuendeleza ustawi wa jamii na kuwawezesha watu kufikia malengo yao," alisema.

Akizungumzia mafanikio hayo ya NMB, Mhariri Mkuu wa Euromoney, Louise Bowman, alipongeza benki hiyo kwa kuwa na mfumo madhubuti na wa kuigwa wa kidigiti na mawakala ambao umechangia asilimia 96 ya miamala yake kufanyika nje ya matawi.

"NMB sasa ina zaidi ya mawakala 28,000 kulinganishwa na chini ya 19,000 iliyokuwa nao mwaka 2022, na imeanzisha kampeni ya kidigiti ili kuongeza ufahamu wa bidhaa zake za kidigiti ikiwamo mikopo midogo ya kidigiti," Louise alisema.




Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali, Alfred Shao (wa pili kushoto), akiwa pamoja Mhariri Mkuu wa Jarida la Kimataifa la Euromoney, Louise Bowman (kulia) na Ed Balls (kushoto) baada ya kupokea tuzo ya Benki Bora Tanzania 2024 kutoka Jarida la Kimataifa la Euromoney lenye makao makuu yake jijini London – Uingereza. Benki ya NMB ilipokea tuzo tano; Benki Bora Tanzania 2024, Benki Bora Mifumo ya ESG Tanzania 2024, Benki Bora ya Kidijiti Tanzania, Benki Bora ya Wateja Maalum na Wateja Wenye Mali katika kilele cha tuzo za Euromoney zilizofanyika nchini Uingereza. Wa pili kulia ni Meneja Mwandamizi wa Idara ya Uhusiano na Wawekezaji, Edgar Ndani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia kugharamia tiba ya mtoto aliyejeruhiwa na mfanyakazi wa ndani

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema atalipia gharama za matibabu ya mtoto Maliki Hashimu (5), mkazi wa Goba, mkoani Dar es Salaam, anayedaiwa kujeruhiwa koo na mfanyakazi wa ndani (house girl).

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu aliyasema hayo jana baada ya kutembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam ambako mtoto huyo yuko chini ya uangalizi maalum.

Tukio la kujeruhiwa mtoto huyo kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, lilitokea usiku wa Julai 15 mwaka huu na kuripotiwa siku iliyofuata.

Kutokana na majeraha makubwa aliyopata baada ya kukatwa na kitu chenye ncha kali shingoni kilichotenganisha njia ya hewa chini ya sanduku la sauti, mtoto huyo alifikishwa MNH - Mloganzila.

Baadaye mtoto huyo alihamishiwa MNH - Upanga kwa ajili ya matibabu zaidi kwa kuwa baada ya kujeruhiwa kulisababisha ashindwe kupumua, kuongea na kupata maumivu na kupoteza kiwango kikubwa cha damu.

MNH kupitia wataalamu wake tayari wamemfanyia upasuaji mkubwa mtoto huyo, ukichukua saa nne kurekebisha njia ya hewa, sanduku la sauti, matezi yaliyojeruhiwa na kutibu jeraha la nyuma ya shingo.

Wataalamu hao walibaini jeraha la mbele ya shingo liliharibu tezi la mbele (thyroid gland) kwa kulikata katikati na kusababisha mtoto huyo kuvuja damu kwa wingi, kupata maumivu makali kutokana na kukatwa sehemu iitwayo (trachea) ambako hewa hupita inapotoka katika mapafu.

Tangu Jumatatu iliyopita, mtoto huyo yuko chini ya uangalizi maalum akiendelea kupata matibabu kutoka kwa madaktari bingwa wa hospitali hiyo.

# Manispaa yafafanua waliokutwa na ugonjwa wa kuhara, kutapika

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

BAADA ya Nipashe kuibua changamoto ya ugonjwa wa kuharisha na kutapika uliokumba maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro na kusababisha Kituo cha Afya Sabasaba kuzidiwa wagonjwa, uongozi wa Halmashauri ya Manispaa hiyo umetoa ufafanuzi kuhusu suala hilo.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Focus Matawa, alisema mwishoni mwa wiki kuwa wagonjwa wote waliokuwa wamelazwa kituoni huko na baadaye kuhamishwa kwa gari ya wagonjwa usiku kupelekwa kambi maalum ya wagonjwa wa kipindupindu iliyoko Mazimbu, tayari wameruhusiwa kutoka kambini.

Alisema wanaendelea na uchunguzi wa kitaalamu kuhusu sampuli ili kubaini kwa kina chanzo cha tatizo, wakati huo wakiendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhusu maendeleo yao kiafya. Mganga Mkuu pia alisisitiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kukabiliana na changamoto za magonjwa ya aina hiyo ikiwamo kutilia mkazo suala la usafi. Dk. Matawa alisema majibu ya sampuli za wagonjwa wa aina hiyo huchukua zaidi ya saa 48, ili kubaini ugonjwa sahihi uliowakumba.

Nipashe ilibaini maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro kukumbwa na tatizo la wananchi kuhara na kutapika maji yanayofanana na dalili za ugonjwa wa kipindupindu, ikiwamo familia moja ya watu watatu kutoka eneo la Yespa, Kihonda, mjini hapa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati kwa waamuzi nao kujiweka fiti Ligi Kuu

**HIKI** ni kipindi ambacho timu zote za Ligi Kuu Tanzania Bara zinafanya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Kuna ambazo zimesafiri kwenda nje ya nchi, zingine zikitoka ndani ya mikoa yao na kwenda mikoa mingine, lengo likiwa ni lile lile kuandaa mazingira ambayo yanaweza kuwafanya makocha kufanya kazi zao kwa utulivu na ufanisi.

Ndicho kipindi ambacho wanafanya kazi kubwa kuviandaa vikosi vyao kuanzia utimamu wa mwili, pumzi, stamina, ufundi na mifumo, vitu vyote hivyo vinatarajia kutumika msimu mzima.

Nasema hivi kwa sababu najua kutokana na ratiba zilivyo, sidhani tena kama makocha wanaweza kupata muda huo tena, kwani kazi yao kubwa itakuwa tu ni kuikochi timu kwenda kucheza kulingana na jinsi mpinzani wao anavyocheza, kusafiri na kuweka miili sawa. Hawatopata tena muda mrefu wa kufundisha kama huu.

Kwa sasa wapo kwenye kazi ngumu wakihangaika kuziweka timu zao kwenye hali nzuri wakitegemea kupata matokeo mazuri uwanjani.

Tahadhari tunaipeleka kwa waamuzi kuwa makini mno kwenye maamuzi yao msimu ujao ili kila mmoja avune alichopanda na si vinginevyo.

Tumeshuhudia huko nyuma baadhi ya maamuzi yamekuwa wakiumiza makocha, wachezaji na mashabiki wa timu zao, hivyo kuonekana kama walichokifanya katika maandalizi kama haya ni kazi bure.

Baadhi ya waamuzi wamekuwa wakishindwa kutafsiri vema sheria 17 za soka kwa bahati mbaya au makusudi, hivyo kuzinyima pointi timu ambazo zilitakiwa kushinda, na kuzinufaisha zisizostahili kwa sare ama ushindi.

Matokeo yake baadhi ya makocha wamekuwa wakitimuliwa kazini wakati mwingine si kwamba uwezo wa kufundisha ni mdogo, bali kunyongwa na baadhi ya maamuzi ya waamuzi.

Msimu uliopita jumla ya makocha 18 walitimuliwa kwenye Ligi Kuu Bara kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kufanya vibaya, lakini ukiangalia wapo ambao waliathiriwa na maamuzi ya waamuzi.

Kwa bahati mbaya sana waamuzi wao husimamishwa kwa mechi kadhaa kabla ya kurudishwa baadaye, lakini makocha wakishatimuliwa inachukua muda mrefu kupata timu.

Tunajua kuwa msimu ujao kutakuwa na Video ya Kuwasaidia Waamuzi (VAR), kufanya maamuzi sahihi, lakini tunatambua kwamba si kila tukio ni lazima aende akaangalie, lakini pia wanaoiongoza VAR ni watu, hivyo pamoja na kuwapo teknolojia hiyo, bado wanatakiwa kuwa makini na uchezeshaji, kwani kawaida kusikia hayo ni makosa ya kibinadamu.


Inaumiza na kukatisha tamaa makocha wanaotumia muda mrefu kuandaa timu, tena wengine wakitoka kabisa nje ya nchi au ya mikoa yao kwa ajili ya kukiweka fiti kwa muda mrefu wa wiki nne mpaka sita, lakini mwamuzi anatumia dakika 90 tu kuweza kumnyima ushindi kocha anayeonekana amemshinda mwenzake kwa mbinu.

Wakati makocha wapo kazini kwa sasa, tunataka waamuzi nao wawe mazoezini na kupata semina zaidi ili kuwa fiti kimwili jambo litakalowasaidia wasipitwe sana na matukio kutokana na kasi ya mpira, pia kuwa waadilifu na kuiacha mechi kujicheza yenyewe bila kulazimisha mambo.

Na hii itakuwa ni faida kwa soka la Tanzania kwani kuiacha timu iliyozidiwa mbinu ipoteze mechi kunaisaidia kwenda kusahihisha makosa ili warejee imara, lakini inapopewa ushindi au kubebwa na mwamuzi haiisaidii bali kuwadumaza viongozi, makocha na mashabiki wao kwa kuona wana timu nzuri, kumbe imesaidiwa kupata ushindi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Yatengenezwe mazingira ya kuvutia mashabiki viwanjani

Na Adam Fungamwango

**LICHA** ya kwamba mashabiki wengi nchini kwa sasa wanapenda soka, lakini bado kuna tatizo kubwa la kuingia viwanjani.

Msimu uliomalizika, Yanga iliongoza kwa kuingiza mashabiki wengi viwanjani, kwa mujibu wa takwimu za Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), ikiingiza mashabiki 141,911, ikifuatiwa kwa karibu na Simba ambayo iliingiza mashabiki 112,717.

Ukiifanyia tathmini ya kina idadi hii na jinsi mashabiki wa soka nchini wanavyopenda mchezo huo ni ndogo sana.

Ukitaka kujua hilo, hebu angalia mechi za Matamasha ya Simba Day na Wiki ya Mwananchi ambapo Uwanja wa Benjamin Mkapa hufurika mashabiki wengi ambapo pungufu yake inakuwa ni 50,000, lakini kiwango cha juu kinakuwa ni 60,000 kwa mechi moja tu.

Kimahesabu inaonyesha matamasha hayo mawili ya timu hizo kubwa moja tu ni wastani wa idadi ya watazamaji wa timu zao msimu mzima.

Hii inaonyesha kuwa bado wahudhuriaji mpirani ni wachache sana, japo kuna mwanga tofauti kwa miaka ya nyuma.

Siku hizi unaweza kuona hata kinamama, kinadada na watoto uwanjani, tofauti na zamani ambapo ni zaidi ya asilimia 95 wanakuwa ni wanaume tu.

Kwa ligi ya Tanzania ambayo imevutia wachezaji wengi kutoka nje ya nchi, wenye uwezo mkubwa, huku ikiwa nafasi ya sita kwenye ubora wa Afrika, bado ni mashabiki wachache sana.

Ukitaka kujua hilo ni jinsi wanavyojazana hotelini, kwenye mabaa, majumbani na vibanda umiza kufuatia mechi za soka zinapokuwa zinaonyeshwa kwenye televisheni.

Hata hivyo, kutokana na upenzi wa mpira wa miguu ulivyo kwa sasa, kama juhudi za makusudi zikifanywa, wanaweza kupatikana mashabiki wengi sana kwenye viwanja vya soka, achilia mbali wanaotazama kwenye luninga.

Ilitakiwa baada ya msimu uliopita kumalizika ligi, wadau wangetafuta sababu zinazofanya mashabiki wasipende kwenda viwanjani, japo wanapenda soka.

Wangepata sababu zingefanyiwa kazi kuelekea msimu mpya. Hata hivyo, kwa uchunguzi wangu mdogo nimegundua tatizo hakuna mazingira mazuri yanayowashawishi kwenda viwanjani.

Wenzetu wameshatoka kufanya uwanjani kama polisi au mahakamani ambako unatakiwa kukaa kwa nidhamu iliyopitiliza, badala yake ni burudani kwa kwenda mbele.

Katika viwanja vyetu, mtu akifika uwanjani kwanza kabisa anakutana na mbwa aliyefungwa kwenye mlango wa kuingilia. Milango yenyewe ni michache kiasi cha kuwa na msongamano mkubwa kabla ya kufika ndani, mpaka akiingia yupo hoi.

Hakuna vitafunwa, juisi, vichangamsha mdomo ambavyo vitauzwa kwa bei iliyozoeleka. Hakuna vinywaji vya kuchangamsha mwili. Hakuna anayeruhusiwa kuingia na chupa ya maji, hivyo mtu kukaa muda mrefu bila huduma hiyo, na hata hayo yanayouzwa ndani kwenye glasi nyepesi yanauzwa ghali sana.

Wenzetu viwanja vyao vina migahawa, na mabaa, ambapo yanawezesha mashabiki kuingia mapema, wanakunywa, wanakula, na inakuwa kama mtoko wa familia kiasi hata mtu ambaye si mpenzi sana wa soka anaweza kwenda kwa ajili tu ya mazingira na mahitaji yanayopatikana uwanjani ambayo yanapatikana pia kwenye mabaa na migawaha mingine.

Nadhani wenye mamlaka wakianza kuvitengeneza viwanja kuwa kama sehemu ya mtoko wa kifamilia, ndipo vitaanza kuvutia watu kujazana viwanjani.

Kuwe ni vivutio na viwezeshi vingine zaidi ya mpira kama vyakula, maji, juisi, vitafunwa, mishkaki, supu, tena maeneo yote na si kwa ajili ya wale wa VIP pekee, vikiuzwa kwa bei ya kawaida tu ya kumwezesha shabiki yeyote kuweza kununua. Hapo tutakuwa tumepiga hatua kubwa ya kushawishi watu kwenda viwanjani.



# Aweso kupeleka wataalamu kwenda kutatua kero Kisarawe

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso (pichani juu), ameahidi kuwa leo anatuma wataalamu kutoka ofisini kwake kutembelea maeneo yenye kero ya wananchi kukosa maji katika Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani ili kufikishwa maji.

Aweso alitoa ahadi hiyo juzi baada ya kupigiwa simu na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti, alipokuwa kwenye mkutano na wananchi wa Kata ya Kiluvya ambao wengi wao walielezea kero ya kutokuwa na uhakika wa kupata maji katika maeneo yao.

"Leo ni Jumamosi, Jumatatu (leo) nitatuma wataalamu watafika hapo Kisarawe kukagua maeneo yenye changamoto ya maji na hatua nyingine zitafuata kuondoa kero hiyo," Waziri Aweso alisema.

Mmoja wa wakazi wa Kiluvya, eneo la Majumba Sita, Rose Msokele alimweleza Mkuu wa Wilaya huyo kwamba maji wanayotumia hivi sasa ni ya kutoka bwawani ambayo si salama kwa afya zao.

Baadhi ya wananchi wa Makurunge pia walielezea kero hiyo ya kutopata majisafi na salama, wakibainisha kuwa wanafunzi wa shule yao ya msingi wanalazimika kwenda shuleni wakiwa na kila siku.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Magoti, alisema mikutano hiyo ya kusikiliza kero ni endelevu ili kutafuta ufumbuzi kwa wananchi ambao wanakutana na vikwazo vya maendeleo.

Magoti pia aliagiza watendaji wa kata zote za wilaya hiyo kuhakikisha wanatenga siku ya Jumanne kusikiliza kero za wananchi na maofisa tarafa kutumia siku ya Jumatano na katika ofisi yake atatumia siku ya Alhamisi kusikiliza kero zilizoshindikana kwenye ngazi za chini.

Alisema kwa kufanya hivyo wataondoa malalamiko ya wananchi katika maeneo yao ambayo yamekuwa yakisababisha baadhi ya lawama kutupiwa viongozi.

Kutokana na kero ya barabara iliyoainishwa kwenye mkutano huo, Mkuu wa Wilaya huyo, aliagiza Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kufanyia kazi kwa haraka maeneo ambayo yameshatengewa bajeti.

Pia alielekeza TARURA kuhakikisha makandarasi walioshindwa kutekeleza kazi zao kwa ufanisi kwa mwaka 2023 wasipewe kazi nyingine kwa kuwa wataendelea kusababisha kero kwa wananchi ambao wamelalamikia kukwama kusafiri kupitia baadhi ya barabara kipindi cha mvua.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga, Mhandisi Godfrey Hilly (kulia) pamoja na Mkurugenzi wa Kampuni ya STC Construction Co. Ltd, Allan Makame (kushoto), wakionesha nyaraka zao baada ya utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji wa uboreshaji wa miradi ya maji kwa fedha za Hatifungani, iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Tanga. Katikati ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akishuhudia. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Pinda atoa angalizo uchochezi CCM

**Na Munir Shemweta,** MLELE

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (pichani), Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, ametoa angalizo kwa wanachama wa chama hicho wanaotaka kugombea nafasi yoyote, wajiepushe na maneno ya uchochezi yanayoweza kuharibu uhusiano baina yao.

Pinda alitoa angalizo hilo juzi wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa CCM wakiwamo madiwani, viongozi wa kata na wazee katika Halmashauri ya Mpimbwe, wilayani Mlele, mkoani Katavi.

Alisema kwa yeyote anayetaka kugombea nafasi ya uongozi, ni vizuri akawa mwangalifu na maneno ya uchochezi aliyoyaeleza kuwa wakati mwingine yanaweza kuwaletea tabu wakati haipo.

"Chondechonde, usije ukaingia katika ugonjwa, unakaa unakuzungusha kichwa kwa sababu kuna mtu kaja kukwambia 'eeh kuna mtu fulani anakusema vibaya'.



"Sasa hujathibitisha unaanza kutembea nayo na wewe usiende hivyo, kwenye siasa hatuendi hivyo," Waziri Mkuu mstaafu Pinda alitoa hadhari.

Aliwataka wanapopelekewa maneno kuyapokea na kutulia huku wakijaribu kuyachunguza ili kuona ukweli au uongo kwa kile wanachoambiwa na kuweka wazi kuwa wengi huponzwa na maneno.


Alisisitiza wana CCM wanapaswa kupunguza maneno ya uchochezi yatakayosababisha kukwaruzana pasi na sababu ya msingi.

Mbunge wa Kavuu, Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema kuwa hali ya kisiasa ndani ya jimbo lake iko shwari na amekuwa anafanya vikao vya mara kwa mara kwa wananchi wa rika zote kupitia kata za jimbo hilo.

Hata hivyo, mbunge huyo aliweka wazi kuwa wakati mwingine kwa namna moja ama nyingine ameshindwa kumfikia kila mwananchi jimboni huko kutokana na idadi kubwa ya wakazi wake inayoongezeka siku hadi siku.

Alibainisha kuwa kupitia Wizara yake ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wako mbioni kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa kila kijiji ili wananchi wapate hati milki za ardhi na kuzitumia kwa mambo ya misingi ikiwamo kuchukua mikopo benki.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza (kulia), akizindua hifadhi mpya ya Rufiji, Mafia, Kibiti na Kilwa (RUMAKI) ambayo imetambulika rasmi kimataifa. Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki wilayani Rufiji Mkoa wa Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi, wasomi waonywa matumizi dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, amewaonya wanafunzi shuleni, vyuoni na taasisi nyingine za elimu kuacha kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya ili nchi isipoteze nguvu kazi inayotegemewa katika kujenga taifa huku akitaka jamii kushirikiana na serikali katika vita dhidi ya dawa za kulevya.

Alitoa kauli hiyo wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara baada ya kufungua kikundi cha ujasiriamali visiwani Zanzibar ambacho kinajumuisha makundi mbalimbali likiwamo kundi la vijana ambalo limekua likiathirika na matumizi ya dawa za kulevya na wamekua wanatumia kwa njia ya kuvuta puani, mdomoni na kujidunga sindano.

"Ni muhimu kwa jamii nzima kushikamana ili kuweza kupambana na matumizi ya dawa za kulevya, utafiti unaonyesha sasa janga la matumizi ya dawa za kulevya limehamia kwa wanafunzi ambao wengine wana digrii zao, lakini wamejiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya, jambo hili linahatarisha uhai wa taifa kwani vijana ni nguvu kazi ya taifa lolote lile duniani, sisi kwa upande wa serikali tumeunganisha nguvu ya pamoja katika kudhibiti uingiaji wa dawa za kulevya na wito wangu kwa wazazi na wanajamii kuhakikisha wanashirikiana na serikali kudhibiti janga hilo," alisema waziri Masauni.

Masauni pia alizungumzia matendo ya udhalilishaji ikiwamo ulawiti, ubakaji, ushoga ambayo yanaendelea kukithiri huku jamii pamoja na familia zikiendelea kuwaficha watu wenye kujihusisha na matendo hayo na kuiasa jamii kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi waonapo dalili za udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto na makundi mbalimbali.

"Kuna mmomonyoko wa maadili unaopelekea matukio ya ukiukwaji wa maadili hayo ikiwamo unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, ulawiti na ushoga; mambo hayo hayajaisha katika jamii yetu na ni muhimu kwa jamii nzima kushikamana ili kupambana na majanga haya na kumekuwa na desturi kwa baadhi ya watu wanaofanya matendo ya ubakaji na ulawiti hususani ya watoto tunawakumbatia na kuwaficha, imefikia hatua mtu amethibitika kufanya ulawiti, lakini wanamficha katika kuhakikisha yule mtuhumiwa aendi kwenye mikono ya sheria hiyo sio sawa."

Taarifa zinabainisha walevi wa uraibu wa dawa za kulevya wamekuja na mtindo wa kutumia dawa za kutibu binadamu kama mbadala wa dawa za kulevya huku wakichukua dawa aina ya methamphetamine ambayo waraibu uchukua dawa hiyo kuisaga na kuiweka kwenye kijiko huku mshumaa ukitumika kuipasha na mwisho mraibu huvuta moshi unaotokana na uunguaji wa dawa hiyo.

# Naibu Waziri Marekani atembelea Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, anayeshughulikia masuala ya siasa, John Bass, ameanza ziara ya kikazi Tanzania na Chad kuanzia Julai 20 hadi 25, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini, Naibu Waziri Bass atakutana na viongozi waandamizi wa Serikali ya Tanzania na kujadili maeneo ya kukuza ushirikiano rasmi.

Eneo jigine ni maendeleo katika mageuzi ya kisiasa na kiuchumi, haki za binadamu na amani na usalama wa kikanda.

Aidha, Naibu Waziri Bass atakutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa asasi za kiraia kuhusu mwelekeo wa kidemokrasia wa Tanzania.

Kiongozi huyo akiwa nchini Chad, atakutana na kufanya mashauriano na viongozi waandamizi wa nchi hiyo kuhusu vipaumbele vya pamoja.

"Pia ni pamoja na kuimarisha ushirikiano rasmi baina ya mataifa hayo mawili, utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa wakimbizi na jinsi ya kushughulikia mzozo na hali mbaya ya kibinadamu nchini Sudan pamoja na uratibu wa masuala ya kiusalama kikanda," alisema.

# Chanzo taka kuendelea kuzagaa mitaani chatajwa

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa usafi wa mazingira wamesema chanzo cha taka ngumu kuzagaa mitaani ni kutotekelezwa kwa Sheria ya Mazingira, uhaba wa wataalamu wa urejelezaji, kutokuwapo na takwimu halisi za ukusanywaji na usimamizi hafifu katika mnyororo mzima.

Aidha, wameshauri kuwapo na ushirikiano wa karibu kati ya serikali na sekta binafsi na zitungwe kanuni za usimamizi wa taka za plastiki zitakazombana mtengenezaji kuwajibika kuzidhibiti kuzagaa mitaani.

Walitoa maoni hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika kikao kilichowakutanisha manispaa zote za mkoa huo, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), sekta binafsi, wahadhiri wa vyuo vikuu na wakusanya taka, kilichoandaliwa na Shirika la Utu na Mazingira (HUDEFO).

Ofisa Mkuu wa Mazingira Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Injinia Boniface Kyaruzi, alisema licha ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, kuelekeza taka kutenganishwa majumbani ili zikarejeshwe na kutengenezwa bidhaa nyingine suala hilo halitekelezwi. Alisema hali hiyo inatokana na manispaa na viongozi wa mitaa kutotekeleza wajibu wao kwa kusimamia utekelezwaji huo na kusababisha taka nyingi kupelekwa dampo la Pugu ambalo limeshajaa na nyingine kuzagaa mitaani.

Alisema takribani asilimia 75 ya taka zinazozalishwa majumbani ni za vyakula ambazo huweza kutengenezwa chakula cha wadudu na mbolea wakati za chupa huweza kutengeneza bidhaa za mapambo, 'tiles' (vigae) na kama utekelezaji huo ukifanyika kama sheria inavyoelekeza kiasi kidogo kitakwenda dampo.

Alisema hata waliopewa jukumu la kusimamia usafi wa mazingira katika manispaa hawana elimu ya kutosha ya vitendo kuhusu usimamizi wa taka, wengi wakiajiriwa kutoka vyuoni moja kwa moja ambao wamesoma nadharia na si vitendo, hivyo kutosimamia suala hilo ipasavyo.

"Hata hivyo hakuna takwimu sahihi za taka zinazozalishwa na zinazokusanywa, zinazopelekwa dampo, zinazozagaa mitaani, na hii inatokana na kuwa tunategemewa kufanyiwa utafiti na watu kutoka nje ya nchi badala ya sisi wenyewe kufanya," alisema.

Alisema inashangaza viwanda vya kurejesha taka vikilalamika kuwa hakuna malighafi ilhali kila leo taka za vyakula na plastiki zinakwenda kumwagwa Pugu.

Alisema wakati umefika kwa serikali na Watanzania kwa ujumla kuondoa dhana ya utegemezi wa dampo kutupa taka bali waelekeze akili zao kwenye viwanda vya urejeleshaji, ili taka zielekezwe huko na wananchi wanufaike kiuchumi.

Aidha, alishauri pia serikali kufanya kazi kwa ukaribu na kuwawekea mazingira mazuri sekta binafsi ambao ndio wanatekeleza miradi hiyo kwa kiasi kikubwa.

"Lakini pia kuna haja ya kuongeza wataalamu na kupitia mitaala ya vyuoni, ili kozi za urejeleshaji wa taka zifundishwe kivitendo zaidi na kuzalisha wabobevu," alishauri.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Hamudi Majanga, alisema taka za plastiki hasa zile zenye rangi zinazagaa mitaani kwa sababu sheria hiyo haielekezi moja kwa moja namna watengenezaji wa chupa hizo wanavyopaswa kuwajibika kuhakikisha hazichafui mazingira.

Alishauri kuandaliwa kanuni zitakazowabana watengenezaji ili na wao wawajibike ipasavyo katika kutokomeza taka hizo kama vile ilivyofanywa kwenye taka za kielektroniki.

Mwandishi wa habari mmoja alipokuwa akifanya utafiti wa makala yake ya kukithiri kwa uchafu katika masoko katika mkoa huo, aligundua kuwa hakuna ushirikiano kati ya manispaa na viongozi wa masoko hali iliyosababisha kutokuwapo na usimamizi mzuri wa taka.

Alisema hali hiyo inaharibu taswira na hadhi ya masoko na kusababisha magonjwa ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara, pamoja na kuikosesha halmashauri mapato.

Ofisa Mazingira Manispaa ya Temeke, John Meena, alithibitisha kuwa elimu na mwamko ya urejeshwaji wa taka bado ni changamoto kwa wananchi jambo linalochangia taka nyingi kwenda dampo licha ya kuwa na viwanda vya urejeshaji.

Alisema manispaa hiyo inakusanya tani 1,494 za taka kwa mwezi kati ya hizo 1,166 sawa na asilimia 78 hupelekwa dampo na asilimia 22 pekee hurejeshwa.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kurejesha taka na namna zinavyoweza kuwa chanzo cha kujiongezea kipato kwao.

Mratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi kutoka TAMISEMI, Hawa Mwechaga, alisema wanaandaa mkakati wa ngazi ya kati, ambao moja ya maeneo watakayoyapa kipaumbele ni taka ili kuhakikisha jamii inaitumia kama sehemu ya kujipatia kipato.

Alisema kupitia mkakati huo utawatambua wadau wote wanaohusika na taka kuanzia mwokotaji hadi mrejelezaji na kuhakikisha wanakuwa katika mazingira rafiki wakati wanatekeleza majukumu yao.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Waokota Taka Rejeshi Dar es Salaam (MTAWADA), Martha Molel, alisema wanapotekeleza majukumu yao ya kuokota taka za plastiki wanapitia changamoto nyingi ikiwamo kupigwa na kubakwa na watu wenye nia ovu.

# RUWASA, wananchi 'wavutana' kisa maji ya bomba

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

MKWAMO wa utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa maji ya bomba katika Kata ya Tingatinga, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, umeibua mtafaruku baina ya wakazi wa eneo hilo na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA).

Wakazi hao wa Tingatinga, wanadai hawaridhishwi na mwenendo mzima wa utekelezaji wa mradi huo.

Wiki iliyopita, wakazi hao walikusanyika mbele ya ofisi ya Serikali ya Kijiji cha Ngereiyani, kushinikiza mabomba yaliyohifadhiwa kwenye ofisi hiyo kwa muda mrefu bila kusambazwa, wapewe sababu za kutotumika, wakati wao wanakabiliwa na shida ya maji.

Mkazi wa Tingatinga, Sara Emanuel, alisema wanawake na watoto wamekuwa waathirika wakuu wa adha hiyo kwa kuwa wamekuwa wakitembea zaidi ya kilometa 18 kila siku kutafuta maji vijiji jirani vya Wilaya ya Siha, ndiyo maana wanataka kupewa taarifa za nini kimetokea hadi mradi kukwama.

Mkazi mwingine wa kata hiyo, Wandeto Sidaye, alisema uamuzi wao wa kujikusanya ofisi ya kijiji ni kutaka kuishinikiza RUWASA Wilaya ya Longido, kuwaeleza sababu ya kukwama kwa mradi huo. Diwani wa Kata ya Tingatinga, Victor Lenganet, alisema kwa muda mrefu wamefuatilia mabomba hayo wakitaka yatumike kutatua tatizo la maji katika eneo hilo, lakini hakuna kilichofanyika, ndiyo maana wananchi wameamua kuvunja ukimya.

Lenganetnet, alisema licha ya Serikali ya Kijiji na uongozi wa kata hiyo, kuchanga fedha na kukodi katapira la kusaidia kuchimba mitaro ya kulaza mabomba, watekelezaji wa mradi huo ambao ni RUWASA, wameshindwa kuendelea na kazi na wanapouliza hawapewi sababu za msingi.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu madai hayo ya wananchi, Kaimu Meneja wa RUWASA, Wilaya ya Longido, Petro Mchenya, alisema tatizo la kusuasua kukamilika kwa mradi huo, chanzo chake ni mgogoro uliopo kati ya wakazi wa Wilaya ya Siha na Tingatinga.

Alisema mgogoro huo unatokana na wakazi wa Wilaya ya Siha, kugomea mabomba ya mradi huo kupita kwenye maeneo yao kwenda Wilaya ya Longido, jambo ambalo ndilo lililozusha mgogoro kati ya wakazi wa wilaya hizo mbili.

Kwa mujibu wa Kaimu Meneja huyo wa RUWASA, mgogoro huo kwa sasa tayari umekwishapatiwa ufumbuzi na wakati wowote kuanzia sasa, mradi huo utaendelea kutekelezwa.



Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Raymond Mwangwala (kulia), akikabidhi bendera kwa kiongozi wa wapandamlima Kilimanjaro ikiwa ni Kampeni ya GGM Kili Challenge 2024 ya Kampuni ya Dhahabu ya Geita Gold Mining katika lango la Machame kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), mjini Moshi, Kilimanjaro jana. Tukio hilo linashirikisha wapandamlima 52 na waendesha baiskeli 19, kwa lengo la kusaidia juhudi za serikali za kupambana na Ukimwi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wachukua hatua kunusuru vyanzo vya maji

**Na Godfrey Mushi,** MONDULI

WADAU wa mazingira kutoka ndani na nje ya nchi, wameanza kuchukua hatua za kunusuru vyanzo vya maji vilivyoko hatarini kukauka katika misitu ya asili ya Serela na Losimingori iliyoko Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha.

Vyanzo hivyo ambavyo ndiyo tegemeo la maji yanayotumiwa na baadhi ya tarafa za wilaya hiyo, vimeharibiwa kutokana na ukataji wa miti ya asili, kwa ajili ya biashara ya kuuza kuni na ujenzi wa makazi ya jamii za kifugaji za Kimasai.

Kutokana na uharibifu huo, Mkurugenzi wa Shirika la Masai Pastoralist Development Organization (MPDO Lareto), linalofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Baraka Laizer, alisema wamelazimika kuwapelekea wakazi wa kata za Serela na Repruko, mradi wa ufugaji wa nyuki kama chagizo la kiuchumi ili kuacha ukataji miti ndani ya misitu hiyo.

"Tangu tumebuni na kuuleta mradi huu wa ufugaji nyuki katika maeneo haya, wananchi wameacha kufanya uharibifu kwenye misitu ya asili ya Serela na Losimingori.

"Dhamira yetu ni kunusuru mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika eneo hili lenye vyanzo vya maji. Kwa ujumla mradi huu unalenga kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji; ambapo kwa sasa tunafanya kazi ya kuzijengea uwezo kamati zinazoshiriki kutunza mazingira na kulinda vyanzo hivi kwenye vijiji husika," alisema.

Mratibu wa mradi huo unaotekelezwa na MPDO Lareto, Amani Sekino, alisema kwenye mradi huo tayari zaidi ya wanawake 60 wamepatiwa mradi wa ufugaji wa nyuki na wameanza kunufaika kiuchumi.

"Wanawake wa jamii za kifugaji walio wengi, wanategemea kuendesha maisha yao kwa kukata miti ya misitu hii. Kwa hiyo, ili kuwapa motisha ya kuachana na uharibu wa misitu ya Serela na Losimingori na kuvinusuru vyanzo vya maji kutoweka, ndio maana tukaja na mradi huu wa kiuchumi," alieleza Sekino.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo kutoka kikundi cha Enywata Maa, Nalembo Ole Shulu, kutoka Monduli, akieleza namna ulivyoanza kubadili maisha yao kiuchumi, alisema mradi huo umewasaidia kuwa chanzo cha kipato kutokana na kuuza mazao ya nyuki.

Alisema kitaalamu, nyuki huzalisha bidhaa nyingi ambazo zina faida kubwa kiafya pamoja na maendeleo ya kiuchumi, kama vile nta, sumu ya nyuki, maziwa ya nyuki, vumbi, supu yake na gundi.

Alipohojiwa na Nipashe kuhusu mchango wa serikali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Isaac Joseph, alisema halmashauri yao inaunga mkono ujio wa mradi huo, kwa kuwa ni mkombozi wa mazingira yaliyoharibiwa kwa ufyekaji wa misitu kwenye baadhi ya vijiji, ili kuvuna miti ya ujenzi na biashara ya kuni.

# Bil.2/- zakusanywa mapambano VVU, UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KAMPENI ya Kili Challenge, inayolenga kusaidia mapambano dhidi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI imekusanya Dola za Marekani 806,000 (Sh. bilioni 2.15) katika Dola milioni moja iliyolenga kukusanya mwaka huu.

Kampeni hiyo ya kila mwaka inayoandaliwa na Kampuni ya Dhahabu ya Geita Gold Mining (GGM), kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), kupanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kusaidia juhudi za serikali katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

Hayo yamo katika taarifa ya Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Raymond Mwangwala, aliyoitoa mwishoni mwa wiki katika lango la Machame la Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), wakati wa kuwaaga wapanda mlima 52 pamoja na waendesha baiskeli 19 wanaochagiza kampeni hiyo.

Katika taarifa yake, alisema serikali inaona uko mwanga endelevu katika kudhibiti ugonjwa huo nchini.

Mwangala ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Rombo, alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

"Napenda kuwashukuru GGM na TACAIDS, ambao ndio waanzilishi na waratibu wa kampeni hii ya Kilimanjaro Challenge Against HIV and AIDS; ambayo kupitia programu hii, leo kwa furaha kubwa tumekusanyika kuwaaga mashujaa waliojitoa kupanda mlima na kuendesha baiskeli kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

...Napenda ifahamike kuwa lengo kubwa la kutekelezwa kwa kampeni hii, ni kuchangisha fedha kwa ajili ya kuchangia juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Hivyo kupitia programu hii, wadau wanapata fursa ya kuchangia fedha na kufanya utalii katika Mlima Kilimanjaro."

Vilevile, Mwangala, alisema kampeni hiyo pia inalenga kujenga urafiki na ushirikiano na mataifa mbalimbali, ambayo raia wake wanajitokeza kushiriki kupanda Mlima Kilimanjaro au kuendesha baiskeli kuzunguka mlima huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGM, Duran Archery, akizungumza kabla ya kuagwa wapanda mlima hao, alieleza kuwa michango hiyo ni dhamira njema ya GGM katika mapambano dhidi ya UKIMWI nchini. "Tumejizatiti kikamilifu kuhakikisha kwamba Tanzania isiyo na UKIMWI inawezekana, kama kaulimbiu yetu ya mwaka huu inavyosema, hatutakata tamaa, Ningependa kuwatia moyo washiriki wa tukio la mwaka huu, kwamba tuko nanyi kwa moyo na tutakuwa tukiwashangilia njia yote," alisema Duran.

Mbali na hilo, Mkurugenzi huyo wa GGM, aliongeza kuwa lengo la kukusanya fedha kila mwaka, ni kuchangia juhudi za serikali kufikia malengo ya sifuri tatu, dhidi ya UKIMWI.

Malengo hayo, ni maambukizi mapya sifuri, unyanyapaa sifuri na vifo vinavyohusiana na VVU/Ukimwi sifuri.

Awali, Simon Shayo, Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti, anayeshughulikia masuala ya uendelevu na mambo ya ubia (Afrika), alisema kuwa vikundi mbalimbali vimefaidika na kampeni hiyo, wakiwemo watoto wa Kituo cha Moyo wa Huruma cha Geita, kilichoanzishwa mwaka 2006.





# Wafanyabiashara Kabanga walalamika kubaguliwa

**Na Restuta Damian,** NGARA

BAADHI ya wafanyabiashara wa mazao, matunda na bidhaa za viwandani katika mpaka wa Tanzania na Burundi, Kabanga wameiomba serikali kuhakikisha wanaweka usawa kwa wazawa katika fursa za kibiashara sambamba na kutatua kero wanazokabiliana nazo mpakani hapo.

Walitoa ombi hilo juzi katika kikao cha wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kilichoandaliwa na kamati ya kitaifa ya uwezeshaji biashara katika forodha ya mpaka wa Kabanga kikilenga kutafuta ufumbuzi wa matatizo na kusaidia wafanyabiashara kufanya kazi katika mazingira rafiki. Mmoja wa wafanyabiashara hao, Christina George, alibainisha kero wanazokabiliana nazo kuwa ni pamoja na raia wa Burundi kupewa sehemu kubwa ya ajira na uingizaji wa biashara mbalimbali nchini, ambapo wazawa wamekuwa walikutana na vikwazo vya kisheria wanapoingiza hitaji kupeleka bidhaa Burundi.

Alisema, kama wafanyabiashara wanahitaji kupewa fursa sawa kama wanazozipata wenzao kutoka Burundi za kuingiza bidhaa nchini bila vikwazo na wao waweze kutoa nje bila vikwazo vya aina zozote.

Mfanyabiashara wa nafaka, John Ibrahim alisema, uingiaji wa wafanyabiashara wa nje ya nchi bila kufuata taratibu za vibali vya ununuzi wa bidhaa, unakwamisha maendeleo ya wafanyabiashara ambao na wao wanafanya shughuli ya usafirishaji nje ya nchi kwa utaratibu maalumu. Mwenyekiti wa Soko la Kabanga, Samweli George, alisema, wafanyabiashara wa ndani wanapofungua viwanda vya uzalishaji bidhaa hujikuta wanafunga kutokana na kukosa wateja wa kununua kutokana na bidhaa zinazotoka Burundi kuingia nchini kuteka soko.

George alisema, hali hiyo inaleta mdororo kwa wazalishaji wa ndani ambao huzalisha bidhaa zinazofanana na zile zinazoingizwa na wafanyabiashara wa Burundi kwa njia za panya na kupewa vibali au kuwatumia mawakala wa ndani.

Kamshina wa Forodha kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Juma Hassan alisema, tayari amepokea malalamiko hayo na wanayatafutia ufumbuzi ili kuhakikisha kila mfanyabiashara anafuata sheria.

Aidha, alisema kuwa ni wazi kuwa bidhaa zinazoingia bila ya kufuata utaratibu za forodha zinaathiri biashara kwa wafanyabiashara wa ndani, hivyo kamati ya kitaifa ya uwezeshaji biashara italifikisha katika vyombo vya uamuzi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi kadi ya mpigakura, Josephina Sikabwe, mkazi wa Mtaa wa Kawawa Kata ya Kipampa, Halmashauri ya Manispaa Kigoma-Ujiji mkoani Kigoma, baada ya kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura juzi. **PICHA: INEC**

# Nape aagiza kampuni kuunga mawasiliano mnara mmoja

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amewaagiza wamiliki wa kampuni za mitandao ya mawasiliano kuunganisha mawasiliano kwenye mnara mmoja, ambao umejengwa wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Amesema hatua hiyo itawasaidia wananchi waishio maeneo ya vijijini kupata huduma ya mtandao wa uhakika. Alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika stendi ya zamani na kueleza kuwa kukamilika kwa mnara huo kutasaidia kuondoa adha waliokuwa wakikabiliana nayo wananchi wa maeneo hayo.

Alisema kwa sasa hawategemea kusikia kilio hicho cha mtandao kutokana na hatua iliyobainika ni kampuni husika kuunga mawasiliano yake katika minara hiyo na kuwafikishia huduma wananchi.

Kuhusu utapeli wa kimtandao na matumizi ya lugha chafu mitandaoni, Waziri Nape alisema serikali haitoacha kuwachukulia kali za kisheria endapo watabainika.

Akizungumza katika mkutano huo, Mbunge wa Sengerema, Khamis Tabasamu aliiomba serikali kujenga mnara maeneo ambayo mawasiliano yanasuasua, kwani kuna baadhi ya mazingira ukifika hakuna mtandao kabisa hali inayowanya wananchi wa maeneo hayo kushindwa kufanya mambo yao muhimu.

Tabasamu alitaja kata zisizo na mnara pamoja na mawasiliano ya shida wilayani hapa kuwa ni pamoja na Kishinda, Bitoto, Kasenyi na Buzilasonga na kumwomba Nape kufanya utaratibu wa kujenga mnara kwenye maeneo hayo.

Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Tanzania kidijitali ambako Mkoa wa Mwanza umeletewa mnara 170, huku Halmashauri ya Sengerema ikipatiwa minara miwili inayogharimu zaidi ya Sh.bilioni 2.44, lengo likitajwa kuwa ni kuendelea kupunguza tatizo la mtandao katika maeneo yenye adha kubwa.

# Punguzo utitiri wa kodi lawakosha wawekezaji wazawa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAWEKEZAJI wazawa waliowekeza katika sekta ya viwanda nchini wamesema wameanza kunufaika na punguzo la utitiri wa kodi katika bidhaa wanazozitengeneza kufuatia kujiunga na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), hali inayowasaidia kujiimarisha kibiashara na kiuchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na mmoja wa wamiliki wa kiwanda cha utengenezaji wa gundi jijini Mwanza, Kapocha Makongoro alipotembelewa na Meneja wa TIC Kanda ya Ziwa, kueleza namna walivyopata msamaha wa kodi, huku wakipata ondoleo la asilimia 75 ya kodi wanapoingiza mashine nchini.

Aidha, aliiomba serikali iangalie namna ya kulinda viwanda vya ndani ili bidhaa zinazotengenezwa na Watanzania ziweze kupata soko, siyo kuruhusu bidhaa za nje zinazofanana na zinazozalishwa ndani kuingia nchini jambo ambalo linaua soko la mali za Watanzania.

Mkurugenzi wa Utawala na Fedha Kituo cha Uwekezaji Tanzania(TIC), Paschal Maganga, alisema ziara hiyo ni ya awamu ya pili ya kampeni ya kitaifa ya uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani, yenye lengo mahususi la kubadili fikra na mtazamo unaonyesha uwekezaji upo kwa ajili ya raia wa kigeni na siyo kwa Watanzania jambo ambalo siyo sahihi.

Alisema, mwaka 2023 TIC ilisajili jumla ya miradi 526 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 5.72, ikitoa ajira zaidi ya 137,010, Januari 2024 hadi Juni wamesajili miradi 409 yenye thamani ya Dola bilioni 3.09, ikitarajiwa kutoa ajira 121,2029 endapo itatekelezwa ipasavyo.

# Wawatuhumu vigogo kufadhili utoroshaji madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu mkoani Shinyanga, wameeleza namna watu wenye uwezo wa kifedha wanavyofadhili utoroshaji wa madini kwa lengo la kukwepa kodi na kusababisha serikali kukosa mapato.

Wamebainisha hayo katika mkutano wao na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita uliolenga kueleza adha wanazokumbana nazo katika shughuli zao za uchimbaji madini.

Mmoja wa wachimbaji hao, Musa Sospeter alisema ili kudhibiti utoroshaji wa madini unaofanywa miongoni mwao ni vema ukapatikana mtandao unaojihusisha na kufadhili ili kuudhibiti kuanzia kwenye chanzo halisi.

"Mkuu wa Wilaya wapo watu kabisa ambao wanatoa fedha kwa kufadhili kazi hii ya utoroshaji wa dhahabu na miongoni mwetu tunawafahamu ila tunaomba ushirikiano na serikali katika kuhakikisha wanakamatwa watu hawa na kuwajibishwa kisheria," alisema Sospeter.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Winfrida Mrema, aliwataka wachimbaji na wafanyabiashara kuwataja wafadhili kwenye utoroshaji wa madini na kuahidi kuwalinda.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alisema, ofisi yake itaendelea kuona ni jinsi gani ya kuwainua wachimbaji wadogo na kutatua adha wanazozikabili katika kazi yao na kuwataka kuacha tabia ya kujihusisha kwenye vitendo vya utoroshaji wa madini kwani ni kinyume na sheria.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 6 WANAOWEZA KUTWAA BALLON D'OR 2024 UK. 12-13



Nahodha wa Argentina, Lionel Messi akiwa na Kombe la Dunia, akinyanyuliwa juu na wachezaji wenzake baada ya kuiongoza timu yao kutwaa ubingwa huo mwaka jana nchini Qatar. **PICHA: MTANDAO**

# MASHINDANO MAKUBWA MATANO YA SOKA DUNIANI

**LONDON,** England

SOKA ndio mchezo maarufu zaidi ulimwenguni na moja ya sababu za hilo ni idadi kubwa ya mashindano ya kusisimua na yenye mashabiki wengi ambayo hufanyika kila mwaka.

Iwe ni ndani ya nchi, bara au kimataifa, karibu kila siku kuna mechi za mashindano ya kandanda kwa wachezaji na wapenda soka. Kuanzia Ligi ya Mabingwa hadi Kombe la Dunia, kandanda ina mashindano ya kipekee na ya kuvutia katika ulimwengu wa michezo.

Katika makala haya mtandao wa habari za michezo kutoka Uingereza, talksport - inataja orodha ya mashindano matano makubwa ya mpira wa miguu. Tukianzia namba tano:

### Copa Libertadores

Kombe la Copa Libertadores ndiyo mashindano makubwa ya soka kwa ngazi ya Klabu kwa Bara la Amerika Kusini. Mashindano hayo huandaliwa kila mwaka na Shirikisho la Soka la bara hilo, CONMEBOL, na hushirikisha timu 47.

Michuano hiyo huanza Februari na fainali hufanyika katika uwanja tofauti Novemba ya kila mwaka.

Tangu kuanzishwa kwa mashindano hayo mwaka 1960. Klabu ya Independiente ya Argentina ndiyo timu iliyofanikiwa kubeba ubingwa mara nyingi katika historia ya mashindano hayo, ikiwa imeshinda mara saba.

### Copa America

Copa America pia ni mashindano ya mpira wa miguu kwa Mataifa ya Amerika Kusini. Yalianzishwa mwaka 1916, Copa America ndio mashindano kongwe zaidi ya mpira wa miguu duniani.

Kwa aina ya vipaji vinavyooneshwa katika mashindano hayo, Copa America ni mojawapo ya mashindano ya soka yaliyotazamwa zaidi duniani.

Jumla ya mataifa 19 hucheza michuano hiyo huku Mexico na Marekani zinazotokea sehemu ya Kaskazini ya Mataifa ya CONMEBOL, zikishiriki pia.

Baadhi ya wachezaji wakubwa wamecheza kwenye Copa America wakiwamo Lionel Messi, Neymar, Pele na Diego Maradonna. Argentina ndio wanashikilia taji la Copa America kwa sasa baada ya kulitwaa mwezi huu, kwa mwaka 2024.

Argentina ndilo taifa lililofanikiwa zaidi katika michuano hiyo kwa kushinda mara 16. Michuano ya Copa America pia inaalika mataifa kutoka CONCACAF (Asia) kushiriki michuano hiyo. Michuano hiyo imeshirikisha timu za Japan na Qatar. Vilevile Australia na China zimekuwa miongoni mwa waalikwa.

### Ligi ya Mabingwa Ulaya

Ligi ya Mabingwa Ulaya ni mashindano makubwa ya ngazi ya Klabu barani Ulaya. Ni michuano ya kila mwaka inayozikutanisha timu bora kutoka ligi za Ulaya. Idadi ya timu kutoka kila nchi inatofautiana kulingana na nafasi ya ligi kwa mujibu wa viwango vya UEFA.

Ligi Kuu ya England, ndio ambayo mara nyingi huingiza timu nyingi, timu nne zikiingia kila mwaka. Katika mashindano ya 2024/25, Klabu za Arsenal, Manchester City, Liverpool, na Aston Villa zitacheza.

Michezo ya mashindano hayo huchezwa katikati ya wiki. Hatua ya makundi huanza Septemba, na hatua ya mtoano huanza Februari na fainali hufanyika Mei.

Real Madrid ndio klabu iliyofanikiwa zaidi katika historia ya mashindano hayo, na kushinda mara 14. Liverpool ndio klabu iliyofanikiwa zaidi ya England kwa kushinda mara sita.

### Michuano ya Euro

Hii huchezwa kila baada ya miaka minne, mwaka huu mashindano hayo yanayozikutanisha timu za Mataifa ya Ulaya (Euro), yamefanyika nchini Ujerumani na Hispania imeibuka mshindi.

Euro hukusanya baadhi ya wachezaji bora kote Ulaya. Mashindano hayo huwa na watazamaji wengi. Mashindano ya kwanza ya kimataifa ya Ulaya yalifanyika mwaka 1960 huko Ufaransa.

Mashindano kumi na saba yamefanyika. Hispania imeshinda mataji manne, Ujerumani wameshinda mara tatu, Italia na Ufaransa wameshinda mara mbili, na Umoja wa Kisovieti, Czechoslovakia, Uholanzi, Denmark, Ugiriki na Ureno zote zimeshinda mara moja kila moja.

Mnamo 2014, mashindano yalipanuka kutoka timu 16 hadi 24, lakini kupanuka huko hakukupunguza kushuka kwa ubora wa mashindano hayo.

### Kombe La Dunia

Kombe la Dunia la FIFA linaendelea kuwa shindano namba moja na kubwa zaidi katika soka ulimwenguni kwa sasa. Hukutanisha wanasoka bora kutoka kote ulimwenguni.

Baadhi ya wanasoka bora duniani wamecheza, wakiwamo Zinedine Zidane, Cristiano Ronaldo, Rivaldo, Diego Maradonna na Pele. Kombe la Dunia la FIFA linaendelea kuwa mashindano ya soka yanayotazamwa zaidi na kufuatiliwa zaidi.

Yalifanyika kwa mara ya kwanza 1930, huko Uruguay na hufanyika kila baada ya miaka minne isipokuwa 1942 na 1946 kwa sababu ya vita ya pili ya dunia.

Argentina waliibuka kuwa mabingwa wa Kombe la Dunia 2022 kwa mara ya tatu baada ya kuishinda Ufaransa kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya mwisho iliyofanyika Qatar.

## ISIKUPITE

ARSENAL, Chelsea na Barcelona zote zinatamani kupata huduma ya winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams ambaye mkataba wake una kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa Euro milioni 58, lakini kocha wa timu hiyo, Ernesto Valverde havutiwi kumuuza.



## Extra Time

# WACHEZAJI 6 WANAOWEZA KUTWAA BALLON D'OR 2024





Lamine Yamal (kushoto) na Rodri wakiwa na tuzo zao, mchezaji bora kinda wa michuano ya Euro na mchezaji bora wa mashindano hayo. **PICHA: MTANDAO**

**PARIS,** Ufaransa

WACHEZAJI watakaoteuliwa kuwania Tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia watatangazwa Septemba 4, mwaka huu. Msimu wa 2023-24 na mashindano makubwa ya msimu huu wa majira ya joto ni mambo yatakayozingatiwa.

**Vinicius Junior wa Real Madrid na Jude Bellingham, wameshindwa kutwaa mataji ya kimataifa wakiwa na Brazil kwenye Copa America na England kwenye Euro 2024, bila shaka hilo limefungua mlango kwa wachezaji wengine pia.**

BBC Sport inawaangalia wachezaji sita wenye uwezo wa kushinda tuzo hiyo Oktoba 28, mwaka huu, mjini Paris nchini Ufaransa.

### Vinicius Junior (Real Madrid, Brazil)

Amecheza michezo 49, amefunga mabao 26, amepiga pasi za mwisho 11, makombe ni La Liga, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Super Cup.

Winga wa Real Madrid, Vinicius mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akitajwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or kwa muda mrefu baada ya kuisaidia timu yake kushinda La Liga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alimaliza msimu akiwa mfungaji bora wa Real Madrid kwa mabao 24 na pasi za mabao 11.

Kama Brazil ingeshinda Copa America pengine angekuwa na uhakika wa kutwaa tuzo hiyo - lakini walitolewa katika robo fainali kwa mikwaju ya penalti na Uruguay, mchezo ambao Vinicius aliukosa kwa sababu ya kufungiwa baada ya kupewa kadi mbili za njano katika hatua ya makundi.

Mbrazil wa mwisho kushinda Ballon d'Or alikuwa Kaka mwaka 2007, na Neymar pekee ndiye aliyemaliza katika nafasi tatu za juu tangu wakati huo.

### Rodri (Manchester City, Hispania)

Amecheza michezo 63, amefunga mabao 12. Ametoa pasi za mwisho za magoli 14. Makombe aliyobeba ni Ligi Kuu England, Uefa Super Cup, Klabu Bingwa Dunia na Euro 2024.

Kiungo wa kati Rodri mwenye umri wa miaka 28, ana mataji manne ya Ligi Kuu England, Uefa Super na Klabu Bingwa Dunia akiwa na Manchester City, na kisha Euro 2024 akiwa na Hispania.

Alitoka nje ya uwanja akiwa ameumia wakati wa mapumziko kwenye fainali ya Euro dhidi ya England, lakini tayari alikuwa amefanya vya kutosha kutangazwa mchezaji bora wa michuano hiyo.

Hakuna mchezaji wa Manchester City ambaye amewahi kushinda Ballon d'Or akiwa na klabu hiyo.

### Jude Bellingham (Real Madrid, England)

Michezo aliyocheza ni 54. Mabao kafunga 27. Katoa pasi za mwisho 16. Makombe aliyoshinda ni La Liga, Ligi ya mabingwa Ulaya na Super Cup.

Kiungo wa kati wa England Bellingham mwenye umri wa miaka 21, alikuwa na msimu mzuri akiwa na Real Madrid kutokana na uhamisho wa msimu uliopita kutoka Borussia Dortmund.

Alimaliza akiwa na mabao 23 - ikiwa ni pamoja na ushindi wa dakika za lala salama katika mechi zote mbili za La Liga akiwa na Real Madrid- na pasi za mwisho 13 kwa klabu yake waliposhinda Ligi ya Hispania na ile ya Mabingwa Ulaya.

Wakati wake wa kuvutia zaidi kwenye Euro 2024, ulikuwa mpira wa juu wa dakika za majeruhi, bao alilofunga dhidi ya Slovakia hatua ya 16-bora.

Kama angeiwezesha England kushinda katika fainali dhidi ya Hispania, huenda angekuwa mshindi wa kwanza wa Ballon d'Or kutoka England tangu Michael Owen mwaka 2001.

### Dani Carvajal (Real Madrid, Hispania)

Michezo aliyocheza ni 54. Mabao aliyofunga ni saba. Pasi za mwisho alizotoa ni nane. Makombe ni LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Super Cup na Euro 2024.

Beki wa kulia Carvajal mwenye umri wa miaka 32, ni mmoja wa wachezaji 12 waliocheza na kushinda fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ubingwa wa Euro katika msimu mmoja.

Aliifungia Real Madrid bao la kwanza katika ushindi wa fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Borussia Dortmund - na pia aliifungia Hispania dhidi ya Crotia katika mechi ya makundi ya Euro 2024.

Kama atashinda atakuwa beki wa pembeni wa kwanza kushinda Ballon d'Or.

### Lamine Yamal (Barcelona, Hispania)

Michezo aliyocheza ni 64. Mabao aliyofunga ni 10. Pasi za mwisho alizotoa ni 14. Kombe ni Euro 2024.

Winga wa Barcelona, Yamal tayari alikuwa na msimu mzuri kwa kijana mwenye umri wa miaka 16, wakati akicheza mechi 50 za klabu, akafunga mabao saba na pasi za mwisho saba.

Kwenye Euro 2024, aliufanya msimu wake kuwa wa kuvutia zaidi kwa mchezaji wa umri wake.

Pasi za mwisho nne nchini Ujerumani zilikuwa muhimu kwenye rekodi ya michuano hiyo ya Ulaya - na alifunga bao zuri katika ushindi wa nusu fainali dhidi ya Ufaransa ambalo liliingia kwenye historia.

Mchezaji huyo mwenye umri mdogo zaidi, mfungaji mabao na mshindi katika michuano ya Ulaya - alitimiza umri wa miaka 17, siku moja kabla ya fainali - alitajwa kuwa mchezaji bora chipukizi katika mashindano hayo.

Gwiji wa Brazil, Ronaldo de Lima akiwa na umri wa miaka 21, mwaka 1997, ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kushinda Ballon d'Or.

### Lionel Messi (Inter Miami, Argentina)

Michezo 39 amecheza. Mabao 28 amefunga. Amepiga pasi za mwisho 17. Kombe ni Copa America.

Messi mwenye umri wa miaka 37, ndiye mchezaji aliyefanikiwa zaidi katika historia ya Ballon d'Or, akishinda mara nane - ikiwa ni pamoja na mwaka jana, baada ya kuiongoza Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia.

Alifunga bao moja pekee katika ushindi wa Argentina msimu huu wa majira ya joto, dhidi ya Canada katika nusu fainali ya Copa America, alitoka nje baada ya jeraha kwenye fainali. Kwa ujumla alicheza chini ya kiwango chake.

Messi hajashinda taji lolote akiwa na Inter Miami hadi sasa.

## Nukuu

"Inabakia kuonekana kama De Ligt atakuja. Namfahamu vizuri Matthijs na sitakataa hilo, nilitaka kumsajili miaka miwili iliyopita lakini wakati huo tayari alikuwa mbali sana kujiunga na Bayern Munich (akitokea Juventus), lakini amini usiamini jina lake halikutoka kutoka kwangu katika mchakato (wa kulenga kumsajili)," **Erik ten Hag, akikiri Manchester United wanataka kumsajili Matthijs de Ligt**



"Vinicius Jr ni mchezaji mzuri na nina furaha sana kucheza naye. Pia, Rodrygo na kila mtu. Wachezaji wazuri wameumbwa kucheza pamoja. Kwangu inanibidi nibadilike na kucheza pamoja na Vinicius na Rodrygo ili tusaidiane kuleta ushindi kwa timu yetu," **Mshambuliaji mpya wa Real Madrid, Kylian Mbappe.**



"Nina ndoto ya kurudi Barcelona, lakini haitakuwa kama kocha, nataka kuwasaidia wachezaji kuboresha mbinu zao. Bodi inafanya kazi kwa njia ambayo si nzuri. Katika miaka ya hivi karibuni, tatizo la Barca limekuwa kwamba [Lionel] Messi yuko nje, kwamba mimi niko nje, kwamba Xavi yuko nje... jambo bora zaidi ni kuheshimu magwiji wa klabu. Hiyo ni muhimu zaidi kushindana kwa wachezaji kama Nico Williams," **Kocha wa zamani wa Barca, Ronald Koeman, ambaye kwa sasa anainoa Timu ya Taifa ya Uholanzi**



Nipashe **Spotika**



PRINCE DUBE

# KLABU TANO ZILIZOTIKISA USAJILI LIGI KUU 2024/25

**Na Adam Fungamwango**

DIRISHA la usajili limezidi kunoga, timu zote 16, zimekuwa zikifanya usajili kulingana na mahitaji ya vikosi vyao.

**Hata hivyo, baadhi ya timu zimeonekana kusuasua kwenye soko la usajili, zingine zikisajili wachezaji wa kawaida tu, wengine bila makeke, lakini zipo klabu ambazo zimekuwa zikifanya usajili ambao umeshtua mashabiki wa soka nchini na kuwa gumzo kwenye vyombo vya habari.**

Hapa tunakuletea klabu tano ambazo pamoja na kufanya usajili wake kwa kujiimarisha kwa mapungufu ya msimu uliopita, lakini umeonekana kuwa tishio na kusumbua vichwa vya mashabiki wa soka nchini.

**1. Simba**

Msimu uliopita si tu kupata ubingwa, ilishindwa hata kuipata nafasi ya pili ili kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika. Matokeo yake ikaangukia Kombe la Shirikisho Afrika kwa kushika nafasi ya tatu.

Kutokana na hilo, yamefanyika mabadiliko makubwa sana kwenye kikosi cha Simba. Imeondoa wachezaji wengi hata wale ambao walionekana tegemeo na kusajili wachezaji wengi wa ndani na nje ya nchi.

Kuelekea msimu ujao, imesajili wachezaji wapya 13, saba wageni na waliobaki ni wazawa.

Ndiyo klabu ambayo usajili wake umeonekana kutikisa zaidi kwenye dirisha hilo kutokana na wingi, pamoja na aina ya wachezaji ambao ingawa si maarufu au mastaa sana kwenye soka la Tanzania, lakini wameonekana kufanya vema waliokotoka ikiwamo wengi kuwa ma MVP (wachezaji wenye thamani zaidi) kwenye ligi zao.

Jushua Mutale kutoka Power Dynamos ya Zambia, Steven Mukwala akitokea Asante Kotoko ya Ghana, Jean Charles Ahoa (Stella Adjame, Ivory Coast), Debora Fernandes Mavambo (Mutondo Stars, Zambia) na Augustine Okajepha (Rivers United, Nigeria) na Valentin Nouma (FC Saint Eloi Lupopo, DRC).

Wachezaji sita wazawa waliotangazwa mpaka sasa ni Lameck Lawi kutoka Coastal Union, Abdulrazack Hamza (Super Sports, Afrika Kusini), Valentino Mashaka (Geita Gold), Omari Omari (Mashujaa FC), Kelvin Kijili (Singida Black Stars) na Awesu Awesu (KMC). Kwa mujibu wa baadhi ya viongozi wao ni kwamba huenda idadi ikaongezeka.

**2. Yanga**

Haikusajili wachezaji wengi msimu huu kutokana na kutopoteza wachezaji wake muhimu walioipatia mafanikio msimu uliopita, lakini wachache iliyopata saini zao ni wale mastaa katika soka la Tanzania.

Hilo limefanya usajili wa Yanga nao kuwa wa kushtua, na hasa ilipomsajili Clatous Chama kutoka Simba.

Ni usajili ambao ulizua mshtuko na mashangao mkubwa kutoka kwa baadhi ya mashabiki, wengine waliona kama ni ndoto.

Wakati mjadala mkubwa ukiendelea, ikamtambulisha Prince Dube kutoka Azam FC, na usajili huo kuendelea kuwa gumzo. Wachezaji wengine waliotangazwa na Yanga ni Chadrack Boka kutoka Klabu ya FC Saint Eloi Lupopo, Duke Abuya raia wa Kenya na golikipa Khomein Aboubakar (Singida Black Stars), Aziz Andambwile (Singida Fountain Gate), pamoja na Jean Baleke (Al Ittihad, Libya), ambaye pamoja na kwamba Yanga haijamtambulisha mpaka sasa, lakini amejitambulisha mwenyewe kwa kufunga bao la kufutia machozi juzi katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Augsburg ya Ujerumani iliyochezwa nchini Afrika Kusini, Yanga ikipoteza kwa mabao 2-1.

**3. Azam**

Kwa mara ya kwanza baada ya misimu 10, imepata tena nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

Baada ya kuipata nafasi hiyo ambapo mara ya mwisho ilikuwa msimu wa 2013/14, hivyo Azam FC ikaamua kufanya usajili mkubwa ambao nao ukawa gumzo kwenye mijadala ya soka.

Imefanya usajili wa straika Jhonier Alfonso Blanco, akitokea kwenye Klabu ya Rionegro Aguilas na kiungo mkabaji, Ever Meza wa Leonnes FC, wote ni raia wa Colombia na klabu wanazotoka ni za nchini humo, beki wa kati Yoro Mamadou Diaby (Stade Malien de Bamako, Mali), pamoja na kiungo mshambuliaji kutoka timu hiyo hiyo, Franck Tiesse, wote wakiwa ni raia wa Mali.

Azam pia imesajili Adam Adam kutoka klabu ya Mashujaa FC na kiungo mshambuliaji wa Kimataifa wa Mali, Cheickna Diakite (Real Bamako), kabla ya juzi kufunga usajili wake kwa kiungo mkabaji Mamadou Samake kwa mkataba wa miaka miwili akitokea kwa miamba ya Algeria, CR Belouizdad ya Algeria

**4. Singida Black Stars**

Imefanya usajili ambao unaonekana ni kama wanaitaka nafasi ya tatu au ya nne kwenye Ligi Kuu msimu ujao, lakini kama watakuwa wapo 'siriasi', wanaweza hata kushika nafasi ya pili au ubingwa kabisa.

Kwanza kabisa imemshuka kipa namba moja kutoka Timu ya Taifa ya Sierra Leone, Mohammed Nbalie Kamara, aliyekuwa akiichezea Horoya ya Guinea.

Halafu ikaenda Ivory Coast katika Klabu ya Asec Mimosas na kumsajili beki wa kati Anthony Tra Bi Tra, ikawasajili Edward Manyama na Ayoub Lyanga kutoka Azam, Kennedy Willson (Simba), Metacha Mnata (Yanga), Ibrahim Imoro (Al Hilal, Sudan) na Joseph Guede (Yanga).

**5. Dodoma Jiji FC**

Baada ya kunusurika kushuka daraja au kwenda 'play off', ikaponea katika mechi za mwisho na hasa baada ya Simba kuifunga JKT Tanzania mabao 2-0 katika mechi ya mwisho, ikiinusuru timu hiyo yenye Makao Makuu jijini Dodoma na kuwapeleka maafande katika mechi za mchujo, kuelekea msimu ujao inaonekana imejifunza kitu.

Nacho ni kufanya usajili wa wachezaji mahiri, wakubwa na wenye uwezo. Ni moja kati ya timu za madaraja ya kati iliyofanya usajili mkubwa ulioshtua wengi.

Imemtwaa kipa mahiri aliyoibeba sana Kagera Sugar msimu uliopita, Allain Ngeleka, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Pamoja naye, imewatwaa Ibrahim Ajibu kutoka Coastal Union, Reliants Lusajo (Mashujaa FC), Dickson Mhilu ambaye amewahi kuichezea Simba, akitokea Kagera Sugar na wengineo.

**JE, WAJUA?**



JACK Grealish, Kalvin Phillips, Julian Alvarez na Matheus Nunes ni wachezaji wanne wanaopewa nafasi kubwa ya kuondoka Machester City majira haya ya joto ili kutoa nafasi kwa usajili mpya.

HABARI KITAIFA

# Jafo: Nitavilinda viwanda ili vitoe ajira

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, ameahidi kuvilinda viwanda vyote nchini, ili viendelee kutoa ajira kwa vijana na hivyo kuwapunguza presha baada ya kumaliza elimu ya juu na ya kati. Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Kampuni ya Alliance One, ambayo inamiliki kiwanda cha kuchakata tumbaku kilichopo eneo la Kingolwira katika Manispaa ya Morogoro.

Akiwa kiwandani hapo, Dk. Jafo alipokelewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Ephraim Mapoore, ambaye alimweleza changamoto kadhaa za kampuni hiyo, ikiwamo ya ukosefu wa maji pamoja na mkanganyiko wa ujenzi wa miundombinu ya umeme kati ya kampuni hiyo na Shirika la Umeme (TANESCO).

"Nimeambiwa kwamba mlijenga njia maalum ya kuwaletea umeme hapa kiwandani kwa makubaliano maalum na Tanesco kwa gharama ya takribani Sh. Bilioni moja kwa maana ya kurejesha fedha hizo kwenye matumizi yenu ya kila mwezi, lakini umeibuka utata ambao unaendelea kwa miaka miwili sasa," alisema Dk. Jafo.

Alisema pia ameelezwa kuhusu changamoto ya maji iliyopo kiwandani hapo, ambapo kwa miaka yote wanatumia maji ya mvua, huku wakiwa hawana miundombinu ya maji kutoka Mamlaka ya Maji ya Manispaa ya Morogoro (MORUWASA) licha ya kuomba kuletewa huduma hiyo kwa miaka mingi lakini bila mafanikio.

Aidha, aliipongeza kampuni hiyo ambayo ilianzishwa mwaka 1998, ambapo hadi sasa imetoa ajira 208 za wafanyakazi wa kudumu na zingine 3,500 za muda mfupi.

Pia aliwaasa viongozi wa kampuni hiyo kuhakikisha kuwa wanalipa kodi zote halali, huku akichukua mapendekezo ya kampuni hiyo kuhusu utitiri wa kodi zinazofanana kwenye sekta ndogo ya tumbaku. Msemaji wa Kampuni hiyo, John Magoti alisema kampuni hiyo imewekeza kiwandani hapo mtaji wa Sh. bilioni 182, inashirikiana na vyama vya msingi vya ushirika 150, vyenye wanachama 13,000 kwenye kilimo cha mkataba wa tumbaku walioko kwenye mikoa ya Kigoma, Tabora, Shinyanga na Mara.

"Kiwanda chetu kina uwezo wa kuchakata kilo milioni 80 kwa muda miezi saba, kikiwa na uwezo wa kuhifadhi kilo milioni 64 kwa wakati mmoja, mwaka huu kampuni imenunua kilo milioni 26 yenye thamani ya Sh. bilioni 162 ambazo zote zimewafikia wakulima," alisema.

Alisema kampuni hiyo ni mlipaji mzuri wa kodi pamoja na michango mbalimbali ya kisheria zikiwamo kodi kwa mwaka huu imelipa Sh. bilioni 4.2 ambazo zimelipwa kwenye halmashauri ambazo zinalima zao hilo.

Kuhusu maslahi ya wafanyakazi alisema kampuni hiyo inalipa kwa wakati.

Kaimu Mkurugenzi wa Kiwanda cha kampuni hiyo, Shepherd Karuwa, alisema waliingia kwenye mkanganyiko na TANESCO kutokana na makubaliano ya kutengeneza miundombinu ya umeme kuanzia eneo la Msamvu mpaka kiwandani hapo.

Amesema kwamba kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano hayo ambao TANESCO wameshindwa kuutekeleza, kampuni ilikuwa inarejesha gharama



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Alliance One Tobacco Tanzania Limited, Ephraim Mapoore (kulia), akifafanua jambo kuhusu uchakataji wa tumbaku kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (wa pili kulia), wakati alipotembelea kiwanda cha kampuni hiyo kilichoko Kingolwira Manispaa ya Morogoro jana. Wa pili kushoto ni Msemaji wa Kampuni hiyo, Wakili John Magoti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi dini watakiwa kuhamasisha uandikishaji wapigakura

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa madhehebu ya dini nchini kuwahamasisha waumini wao kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura, ili wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu 2025.

Pia amewahakikishia Watanzania kuwa uchaguzi huo utakuwa huru na wa haki.

Alitoa rai hiyo juzi kwenye kilele cha Mkutano wa Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Pentekoste Tanzania (CPCT), uliofanyika mkoani hapa.

Alisema viongozi wa dini wanapaswa kuhamasisha waumini wao kujitokeza kujiandikisha ili washiriki kupiga kura kuchagua viongozi wanaowataka.

"Hamasisheni waumini wenu kujiandikisha ili kuchagua viongozi bora na waadilifu watakaowaongoza kama kuna mtu alipiga kura akiwa Manyara sasa upo Dodoma basi unapaswa kwenda kurekebisha taarifa zako ili upate fursa ya kuchagua," alisema na kuongeza:

"Niwahakikishie ndugu zangu uchaguzi utakuwa huru na haki hivyo viongozi wa dini mnapaswa kuendelea kuhamasisha watu kujiandisha ili wachague viongozi ama wao kuchaguliwa". Alisema. Aidha, alitoa wito kwa taasisi za dini nchini kuendelea kushirikiana na serikali katika kutoa mchango kwenye maendeleo.

Majaliwa alisema taasisi za dini zina uwezo mkubwa wa kutoa huduma imara za kiroho na kugusa maisha ya watu katika jamii na kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kisiasa.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema serikali inathamini uwepo na mchango wa taasisi za dini katika kuhubiri amani na utulivu nchini.

Mwenyekiti wa CPCT, Dk. Barnabas Mtokambali, alisema kuwa kupitia madhehebu na wanachama wake wataendelea kushirikiana na serikali katika kuendeleza sekta za elimu na afya.

"Hili siyo tu kwamba linapunguza mzigo mkubwa wa serikali katika kuihudumia jamii kubwa ya Watanzania katika mahitaji husika, bali pia linasaidia kupunguza tatizo kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana," alisema.

Alisema CPCT itaendelea kushirikiana na serikali kuhimiza maadili mema kwa mafundisho ili kupinga wimbi la mmomonyoko wa maadili linaloukumba ulimwengu.

# Viongozi Eswatini watua nchini kujifunza kuhusu mafao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UJUMBE wa watu tisa kutoka Ufalme wa Eswatini wa Waziri wa Utumishi umewasili nchini kujifunza namna Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) unavyoendeshwa.

Akizungumza juzi jijini hapa baada ya kupokea ujumbe huo, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-Razaq Badru, alisema lengo ni kubadilishana uzoefu wa uendeshaji mfuko kati ya nchi hizo mbili.

"Eswatini wapo na sisi hapa Dodoma kujifunza mambo makubwa ikiwamo kufahamu namna ambavyo sisi PSSSF tumeweza kufanya mageuzi makubwa tangu kuanzishwa kwa mfuko, tumezungumza nao kuhusu mageuzi katika huduma tunazotoa kwa wanachama," alisema.

Pia alisema wameelezwa namna ya kusimamia shughuli za uwekezaji ili kuhakikisha kwamba unapowekeza mitaji ya mifuko lazima ielekezwe maeneo yenye tija yanayoweza kuzalisha na yawe na mchango katika maendeleo na uchumi wa nchi.

"Hayo ndio baadhi ya mambo ambayo tumezungumza nayo wayasingatie wakati wakitekeleza mikakati yao ya kuimarisha sekta ya hifadhi ya jamii na kuboresha mfuko wao katika Falme za Eswatini, tutaendelea kuwapa usaidizi wa kitaalam wakati wanatekeleza mikakati hiyo, wametuchagua sisi tufanye hivyo,"alisema.

Waziri wa Utumishi wa Eswatini, Mabulala Maseko alisema wamekuja nchini kupata uzoefu wa namna ambavyo PSSSF imekuwa inapambana kuhakikisha mfuko wake unaendelea kuwa imara na unatoa huduma bora kwa wanachama.

# Mtandao wa kuleta mapinduzi ya kifikra wazinduliwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MTANDAO wa Vijana na Wanawake 'TK Movement' wenye lengo la kuendesha vuguvugu la kujitolea ili kuleta mapinduzi ya kifikra kwa jamii na kuhimiza kushiriki kwenye fursa umezinduliwa mkoani Singida.

Uzinduzi huo umefanyika jana mjini Singida na kushirikisha maelfu ya vijana na wanawake ambao kabla ya kuzinduliwa walifanya maandamano kuzunguka mitaa ya mji wa Singida yakiongozwa na viongozi wa kitaifa na mkoa wa mtandao huo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, akizindua mtandao huo aliwataka vijana kuendelea kulinda tunu za taifa ambazo ni amani, utulivu na uzalendo ili Tanzania iendelee kuwa na amani.

Naye Mshauri wa TK Movement Taifa, Hemed Ali, alisema kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 vijana na wanawake wapo zaidi ya asilimia 70, hivyo ni kundi muhimu katika maamuzi, ujenzi wa jamii bora na maendeleo ya taifa.

Alisema kwa kipindi kirefu vijana na wanawake wamekosa 'platform ' ya kukutana bila kujali itikadi za siasa, dini na ukanda lakini sasa kupitia TK Movement wataweza kukutana kujadili mambo mbalimbali ya maendeleo yakiwamo upatikanaji wa fursa ambazo zitachangamkiwa na makundi hayo kuzipata. Awali Mratibu wa TK Movement Mkoa wa Singida, Sophia Salehe, alisema misingi ya mtandao huo ni utaifa, uzalendo na kujitolea ambapo mtandao utaendelea kuwaelimisha vijana wa kitanzania wawe na ufahamu mzuri wa mambo hayo.

Alisema: "Tunaamini kwamba vijana wenye kuelewa na kuheshimu tunu za taifa, uzalendo na kujitolea ndiyo watakaoivusha taifa kuelekea kwenye kesho iliyo bora kuliko jana na leo hii ni kwa sababu vijana ndiyo nguvu kazi kubwa ya taifa hili."





# Viongozi ushirika wasababisha hasara mil. 440/-, RC atoa agizo

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani hapa kuwasweka ndani viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Kakao wilayani Kyela (KYECU) kwa tuhuma za kuwasababishia wakulima hasara ya zaidi ya Sh. milioni 440.

Viongozi hao wanadaiwa kusababisha hasara hiyo kutokana na taarifa za mnada uliofanyika Julai 15 mwaka huu, kuonyesha zaidi ya magunia 200 ya kakao hayaonekani kwenye maghala ya kuhifadhia licha ya nyaraka kuonyesha kuwa yalipokelewa.

Miongoni mwa viongozi ambao Mkuu wa Mkoa aliagiza wakamatwe ni Mwenyekiti, Evance Mwaipopo na Meneja Julius Mwankenja ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa shughuli za chama.

Homera aliagiza kukamatwa kwa viongozi hao juzi alipozungumza na wakulima pamoja na wadau wa kakao wilayani humo ambapo pia aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuwachunguza viongozi hao.

Alisema hivi karibuni Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa alipofanya ziara wilayani humo aliagiza viongozi hao kuweka wawakilishi kwenye maghala kwa ajili ya kufuatilia takwimu za kakao inayopokelewa lakini hawajatekeleza na hivyo kusababisha upotevu wa mazao kuendelea.

Alisema ili kudhibiti tatizo hilo lisiendelee kutokea kila mnada unapofanyika viongozi wa mfumo wa stakabadhi ghalani na TMS lazima wawepo kwa lengo la kufuatilia kila kinachofanyika.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase alisema upotevu wa magunia hayo ulibainika baada ya mnunuzi aliyeshinda kuanza kuhesabu magunia.

Alisema takwimu zilizokuwa zimetolewa na viongozi hao kwenye mnada ni kwamba magunia yalikuwa 1,915 lakini baada ya mnada kukamilika, mnunuzi akaamua kuhakiki na ndipo akabaini kuwa kuna upungufu wa zaidi ya magunia 200.

Alisema tatizo lililopo ni viongozi hao hawana wawakilishi kwenye maghala licha ya kuagizwa kufanya hivyo na kwamba hali hiyo inasababisha baadhi ya wasimamizi wa maghala kuingiza takwimu za magunia hewa.

"Tunao ushahidi kwamba kwenye maghala hawajaweka wawakilishi kama ambavyo Waziri Mkuu aliagiza, labda kama wao huyo mwakilishi anakuwapo baadhi ya siku watuambie lakini sisi tumefuatilia na tumebaini hivyo," alisema Josephine.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa KYECU Mwaipopo alisema wao kwenye kila ghala kunakuwapo na wawakilishi ambao wanafanya kazi ya kuhakiki kila mzigo unaoingia.

Alisema tatizo linalosababisha upotevu wa mazao ni uwepo wa watunza ghala zaidi ya mmoja akidai kuwa wengine sio waaminifu na hivyo wanaingiza takwimu hewa.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo, alisema tatizo lililobainika ni kwamba viongozi hao wanazichukua taarifa zilizoandaliwa kwenye maghala na kuziingiza kwenye mfumo bila kuhakiki usahihi wake.

Alisema pamoja na tatizo hilo walilobaini pia watafuatilia na mifumo mingine inayotumiwa na viongozi hao ili kubaini sababu zingine.



Mmoja wa wajasiriamali wa Soko la Sido jijini Mbeya wanaochoma viazi vitamu, akiendelea kuwahudumia wateja wake hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Walalamika shule kukosa mwalimu wa kike

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHULE ya Msingi Izumbwe Two iliyopo Kata ya Iwiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, haina mwalimu hata mmoja wa kike, hali ambayo inadaiwa kusababisha wanafunzi wa kike kutohudumiwa vizuri wanapokuwa kwenye siku za hedhi.

Kutokana na hali hiyo, wazazi wameiomba serikali kupeleka mwalimu hata mmoja wa kike ili awasaidie watoto wao wanapokuwa kwenye hali hiyo, wakidai kuwa huwa wanashindwa kuwaambia walimu wao wa kiume.

Waliwasilisha ombi hilo wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika kijiji hicho cha Izumbwe Two.

Mmoja wa wananchi hao, Jamila Mwale alisema wanafunzi hasa wa darasa la sita na la saba huwa wanakosa msaada na hivyo hilazimika kutohudhuria shuleni.

Alisema jirani na shule yao kuna zahanati ya kijiji ambayo pia ina watumishi wote wa kiume hali ambayo inasababisha watoto kukosa msaada wa karibu. "Tunaamini kwamba hata kama mwanafunzi atamweleza mwalimu wake wa kiume bado hawezi kumuandaa vizuri, sasa tunashindwa kuelewa kwamba serikali haitambui mazingira hayo kwa watoto wetu?" alihoji Mwale.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Tax Kibona alisema mbali na kukosekana kwa walimu wa kike kwenye shule hiyo, pia miundombinu ya shule hiyo sio rafiki kwa wanafunzi wa kike kujisitiri wanapokuwa kwenye siku za hedhi.

Alisema hakuna chumba maalumu cha wasichana hao kujisitiri kama ambavyo inatakiwa na hivyo akaiomba serikali kuwasaidia kurekebisha mazingira hayo.

Alisema kijiji hicho kina shule mbili za msingi ambazo zote miundombinu yake ni mibovu na kwamba inasababisha hata kiwango cha elimu kuwa chini kuliko maeneo mengine.

"Hili kwetu ni kero kubwa sana, tunakuomba mbunge utusaidie maana watoto wetu wanapata wakati mgumu, wakati mwingine mtoto anaweza akaona ni vema akamwambia mwalimu wake kuliko hata mimi mzazi, sasa kama mwalimu mwenyewe ni wa kiume inakuwa ngumu," alisema Kibona.

Akijibu kero hiyo, Njeza alisema ataliwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo ili ndani ya muda mfupi wapelekewe mwalimu hata mmoja wa kike atakayesaidia kutatua kero hiyo.

Alisema kwa mujibu wa miongozo ya elimu ni kwamba kila shule lazima kijengwe chumba maalumu kwa ajili ya watoto wa kike kujisitiri na hivyo akasisitiza kuwa watakapokuwa wanatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya elimu kwa shule za awali na msingi (BOOST) hilo litazingatiwa.

Alisema atashiriki kwenye ufuatiliaji ili kuhakikisha jambo hilo linatekelezwa na wanafunzi wanasoma katika mazingira ambayo ni rafiki kwao.

# Wazazi watakiwa kutowaficha watoto wenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi wenye watoto wenye ulemavu jijini Mbeya, wametakiwa kutowaficha watoto hao ndani na badala yake watoe taarifa kwa viongozi wa maeneo yao, ili wasaidiwe kupata misaada ya matibabu na huduma zingine muhimu.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Iyela One, Saad Njechele, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anapokea msaada wa kiti mwendo kwa ajili ya watoto wa mtaa wake wenye ulemavu wa viungo aitwaye Ahadi Yusuph.

Kiti hicho ni miongoni mwa viti viwili vilivyotolewa na Taasisi ya Tulia Trust inayomilikiwa na Mbunge Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, kwa ajili ya watoto wa Kata za Iyela na Ruanda.

Njechele alisema kuna baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwaficha watoto wao wenye ulemavu kutokana na kuwa na imani potofu jambo ambalo alisema linawakosesha watoto hao fursa mbalimbali ikiwamo haki ya kusoma na kucheza.

"Semeni tuwatafutie watu misaada maana wapo watu wengi ambao wanatoa misaada ya aina hii, tunamshukuru sana mbunge wetu maana amekuwa kinara wa kutoa misaada hii kwa watu wetu," alisema Njechele.

Diwani wa Kata ya Ruanda, Ruben Kipalule alimshukuru Dk. Tulia kwa msaada huo akidai kuwa kiti hicho kitamsaidia mtoto aliyepatiwa kwenda shuleni na hata kwenda kucheza na wenzie.

Alisema msaada huo ni wa tatu katika kata yake kwa maelezo kuwa awali vilipelekwa viti viwili ambavyo viwili vya awali vlipelekwa katika Mtaa wa Soweto na walichokipokea kwa sasa kimepelekwa katika mtaa wa Ilolo.

Ofisa Habari wa Taasisi ya Tulia Trust, Addy Kalinjila, alisema walipewa maagizo na Dk. Tulia kuwapelekea wahitaji viti hivyo ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

Alisema watoto ambao waliombewa viti hivyo ni wanafunzi na hivyo viti walivyopatiwa vitawasaidia kufika shuleni kirahisi na kuwarahisishia wazazi na marafiki zao namna ya kuwasindikiza mahali popote wanapotaka kwenda.

# Wakulima wa mwani waomba msaada wa watafiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wa mwani Zanzibar wameiomba serikali kuwapatia wataalumu wa utafiti kwa ajili ya kutambua magonjwa yanayothiri zao hilo.

Walitoa ombi hilo wakati wa kikao kilichofanyika Maruhubi visiwani hapa, kilichoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Mipango kwa ajili ya kusikiliza changamoto zinazowasibu wakulima wa mwani, kuzipatiwa ufumbuzi kwa lengo la kuongeza uzalishaji na thamani katika zao hilo.

Wakulima hao walisema kwa kipindi kirefu zao la mwani limekuwa likishambuliwa na magonjwa ambayo yanasababisha kupungua kwa uzalishaji wa zao hilo.

Simni Haji kutoka Kijiji cha Uroa alisema wananunua mbegu za mwani zikiwa katika hali nzuri lakini wakizipanda katika mashamba yao zinakatika na kuoza.

Fatma Ali Rajabu kutoka Kijiji cha Chwaka alisema pia wanaathiriwa na magonjwa ya mwani ambapo kwa sasa baadhi ya wakulima wameacha kulima zao hilo.

Naye Ali Abdalla Ali mkulima wa mwani katika kijiji hicho cha Chwaka alisema lazima hatua za awali zichukuliwe kuangaliwa uwezekano wa kupatiwa mbegu nyingine ili kubaini iwapo wanazotumia kama zinasababisha magonjwa au laa.

Aidha, alitaka kupatiwa mabwana shamba wanaohusika na utaalamu wa zao hilo ili wawe wanawapitia mara kwa mara katika mashamba yao kwa ajili ya kuangalia.

Hata hivvyo wakulima hao walitaka kuongozewa bei ya mwani wakisema wanatumia gharama kubwa wakati wanapolima.

Mkurugenzi wa Uratibu Uchumi wa Bluu, Christopher Muhamdo, alisema lengo la kukutana na wakulima wa mazao ya baharini ni kutanua wigo wa kuwatoa sehemu moja kwenda nyingine ambayo itakuwa na tija zaidi.

Sambamba na hilo alisema serikali imeleta wataalamu kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa kaa na majongoo bahari kutokana na changamoto nyingi zinazojitokeza kwa wakulima ili kuondoa upungufu uliokuwapo.

Ofisa Mkuu wa Uvuvi, Mohammed Soud kutoka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini alisema ushirikiano wa pamoja unahitajika juu ya kudhibiti uvuvi haramu ambao unasababisha kwa baadhi ya samaki kutoweka pamoja na uharibifu wa mazingira.

Alisema serikali inatambua kuwepo kwa changamoto ya bei ya mwani, ndio mana ikaona ipo haja ya kujenga kiwanda cha kusarifu Chwamanangwe Pemba ili kuleta ushindani wa bei kwa serikali na kampuni binafsi.

Veronika Sigalla mwakilishi kutoka UNDP alisema lengo la kukutana na wakulima wa mwani ni pamoja na kuangalia namna ya wakulima hao wanavyolima zao hilo katika kiwango cha kimataifa.

Alisema wakulima wa mwani ni wadau wakubwa katika kuitumia bahari, hivyo aliwataka kutunza mazingira ya bahari ili kuwanufaisha zaidi.

# Wakazi Tumbatu wamkosha Makamu wa Rais

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema ameridhishwa na ushirikiano unaotolewa na wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu kwa makandarasi wanaojenga miradi ya maendeleo kisiwani humo.

Aliyasema hayo katika ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa shule ya sekondari inayojengwa katika Kijiji cha Tumbatu Gomani kisiwani humo.

Hemed alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wa Tumbatu wanapata huduma zote stahiki za kimaendeleo kwa kiwango kinachokubalika sawa na maeneo mengine.

Alisema wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu wana kila sababu ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Dk. Mwinyi ikiwamo za kuwaletea maendeleo endelevu katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu, afya, barabara, umeme na maji safi ili ustawi wa wananchi kuimarika zaidi.

Hemed alisema serikali itahakikisha inazipatia ufumbuzi changamoto zilizomo kisiwani humo ikiwa ni pamoja na kuajiri madaktari wazawa na watumishi wa kada nyingine wanaotoka maeneo hayo, ili kuepusha usumbufu wa kutokupatikana huduma kwa wakati.

Aidha, aliwataka wananchi wa Tumbatu na Wazanzibari kuendelea kudumisha amani na ushirikiano uliopo nchini ili kupata maendeleo endelevu yatakayokuwa na faida kwa vizazi vya sasa na baadaye.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema dhamira ya Rais Dk. Mwinyi ya kuleta mageuzi katika sekta ya elimu mijini na vijijini inaonekana wazi wazi kwa kujengwa shule za kisasa zenye kukidhi mahitaji yote ya kufundishia na kujisomea.

Mkandarasi kutoka Kampuni ya Simba Developers Ltd, Lucas Lucas, alisema licha ya kukabiliwa na changamoto ya usafirishaji wa vifaa kwa ajili ya ujenzi lakini watahakikisha wanakabidhi mradi huo mwezi ujao ili kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo.

Alisema pia watajenga jengo hilo kwa viwango na ubora, litawahudumia zaidi ya wanafunzi 1,890 kwa wakati mmoja.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, akiangalia moja ya vikapu vilivyotengenezwa na Kikundi cha Wazazi cha Wajasiriamali baada ya kukizindua katika eneo la Kilimani, ambacho kinajishughulisha na ushonaji, utengenezaji sabuni na biashara mbalimbali. Tukio hilo la ufunguzi limefanyika Visiwani Zanzibar jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

# ‘Wahitimu wengi kidato cha sita wanauhitaji elimu ya juu’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa kampuni ya mawakala wa vyuo vikuu vya nje ya nchi, Abdulmalik Molel amesema kuna wimbi kubwa la wanafunzi waliohitimu kidato cha sita ambao wanauhitaji wa elimu ya juu.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya Tano ya Wiki ya Elimu ya Juu katika viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar, ambayo yalidumu kwa muda wa siku saba na kufungwa jana na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Abdulgulam Hussein. Alisema kuwa ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita mwaka huu ni asilimia 99 lakini hakuna nafasi ya kutosha katika fani ya sayansi ya afya na uhandisi kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wenye uhitaji wa elimu ya juu. Alisema ni vyema vyuo viliopo nchini kushirikiana na vyuo vya nje kuwa na kampasi zao nchini ili kutoa fursa kwa vijana kupata elimu kwa gharama nafuu.

Pia aliwataka vijana wa kitanzania kuchangamkia fursa za ufadhili wa masomo ya elimu ya juu zinazotolewa ili kupata fursa ya kupata elimu.

“Vijana wengi wanakata tamaa wanapoona maelezo mengi ya fursa za udhamini wa masomo ya juu zinazotolewa, hivyo vijana mnapaswa kuchangamkia fursa hizo na kama wanahitaji msaada wa kufaidika na fursa hizo waje ofisini kwetu tutawasaidia jinsi ya kuomba,” alisema.

Aidha, alisema kampuni hiyo inakusudia kuviunganisha vyuo vya ndani na nje kupeana uzoefu juu ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa wanafunzi wanaomaliza elimu ya juu vyuoni.

Molel alisema nchi nyingi zimekuwa na mifumo mizuri inayotengenezwa katika vyuo ambapo vijana wanapomaliza masomo huajiriwa, lakini kwa hapa nchini hali ni tofauti.

Alisema wameamua kuleta vyuo mbalimbali vilivyopo nje ya nchi ili kuona udahili unafanyika vizuri kwa wanafunzi aliyekuwa na matokeo mazuri ya kidato cha sita na kusoma fani anayoitaka.

Hata hivyo alisema wanatoa udhamini wa asilimia 100 kwa wanafunzi, fursa ambayo wameipeleka katika maonesho hayo lengo ni kuona wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema maonesho hayo yamekuja wakati mwafaka kipindi ambacho tayari matokeo ya wanafunzi wa kidato cha sita yametoka jambo linalowasaidia wanafunzi hao kufika katika mabanda hayo kupata taarifa sahihi.

Aidha, alifurahishwa na mwamko mzuri wa wanafunzi wa Zanzibar ambao wamekua wakiitumia fursa hiyo kufika katika maonesho hayo na kupata maelekezo juu ya fani zinazotolewa na vyuo pamoja na kufahamu njia zinazotumika kujiunga na vyuo.

Baadhi ya wanafunzi waliofika katika maonesho hayo walisema kuna changamoto katika uombaji wa vyuo nje ya nchi, lakini kuja kwa maonesho hayo kuwarahisishia kufanya udahili kwa urahisi.

# Walezi wadaiwa kutelekeza watoto vituoni na kubadili namba za simu

**Na Kulwa Mzee**

MLEZI wa kituo cha kulelea watoto yatima na wanaotoka kwenye mazingira magumu cha Asante, Magreth Edward, amesema walezi kubadili namba za simu baada ya kumkabidhi watoto na wengine kuhama maeneo waliyokuwa wakiishi ni tatizo kubwa kwenye kituo hicho.

Aidha, amesema kwa kuhudumia watoto wenye ulemavu anapokosa 'pampas' (nepi maalum) kwa ajili yao analazimika kuchana nguo kama kanga kwa ajili ya kuwafutia wanapojisaidia.

Magreth aliyabainisha hayo juzi alipokuwa anapokea misaada ya vyakula na vitu mbalimbali kutoka kwa Hussein Hussein ambaye aliadhimisha siku yake ya kuzaliwa kwa kupeleka misaada kwa watoto hao, kula nao chakula na kukata keki.

"Ninalea watoto 23, wa kiume 13 na wa kike 10, miongoni mwao watoto wawili walemavu na watoto wote wamefiwa na wazazi isipokuwa mmoja ndio ametoka kwenye mazingira magumu.

"Aliyetoka kwenye mazingira magumu nilimtoa kwa bibi yake, ili apate chakula mpaka bibi atoke kuokota chupa, baada ya kumchukua nilishangaa yule bibi akahama na nyumba aliuza.

"Huyu mtoto yupo nilimwandikisha shule anasoma, hawa wengine walezi wao hata namba za simu walibadilisha siwapati tena, nasomesha wengine wako shule za msingi na wengine sekondari.

"Pamoja na changamoto za mahitaji kituoni tuna changamoto ya 'pampas' kwa ajili ya kuwahudumia watoto walemavu, zikiniishia nalazimika kuchana kanga nawafutia, naomba msaada tuweze kuwalea hawa watoto," alisema Magreth.

Msimamizi wa kituo hicho, Nurudini Ulaya, alisema kilianzishwa mwaka 2018 maeneo ya Kwakapungu Ukonga kikiwa na watoto 12 wakiwamo wa kike saba na wa kiume watano, lakini sasa hivi kina watoto 23 wa kiume 13 na wa kike 10.

"Changamoto zilizopo kwenye kituo ni kusuasua kwa usajili, tumetakiwa kukarabati jengo, kuweka jiko la kisasa na kubadili nyavu kwenye madirisha.

"Changamoto nyingine eneo dogo watoto wanakosa eneo la michezo, tumepata eneo linauzwa Sh. milioni 10 hivyo tunaomba msaada wa rasilimali fedha ili tuweze kulinunua," alifafanua Nurudini.

Akitoa nasaha kwa watoto hao, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kivule, Amos Hangaya, aliwataka kufanya bidii katika kila jambo wanalofanya na waombe Mungu abariki kazi ya mikono yao.

"Someni kwa bidii, mpendane nyie kwa nyie na msaidiane, Mungu ametaka mpitie hapa mlipo, mnaweza kufanya vizuri sana kupitia hapa," alisema Hangaya.

Hussein Hussein ambaye ni mwanzilishi wa Hussein Foundation, anafanya hivyo kwa mara ya pili kila Julai 19, anapoadhimisha siku yake ya kuzaliwa.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah, akimkabidhi Sh. milioni 30 Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilida Buriani, kwa ajili ya kuwalipia ada madereva 600 ambao watapatiwa mafunzo ya mwezi mmoja katika Chuo cha VETA mkoani Tanga kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kipindupindu chaua, 105 walazwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MTU mmoja amefariki dunia na wengine 105 wanaendelea na matibabu katika vituo mbalimbali vilivyotengwa kufuatia kulipuka ugonjwa wa kipindupindu mkoani Lindi.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mganga Mkuu Mkoa wa Lindi, Dk. Hery Kagya wakati akitoa taarifa kwa Mkurugenzi Huduma za Afya Ustawi wa Jamii na Lishe wa Ofisi ya Rais na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Rashidi Mfaume, aliyekuwa ziarani mkoani humu.

Mkurugenzi Mfaume alikuwa na ziara ya siku tatu kuangalia usimamizi wa shughuli shirikishi za huduma na maendeleo ya afya katika halmashauri tatu za Nachingwea, Ruangwa na Manispaa ya Lindi.

Dk. Kagya, akiwasilisha taarifa katika majumuisho ya ziara ya mkurugenzi huyo, alisema ugonjwa wa kipindupindu uliibuka mkoani Lindi mwanzoni mwa mwezi huu, na mtu mmoja amefariki dunia na wengine wamelazwa kwenye vituo saba vilivyoanzishwa.

Alieleza kwamba hadi kufikia Julai 15 mwaka huu, wagonjwa waliokuwa kwenye vituo hivyo ni 105 katika halmashauri tatu kati ya sita za Mkoa wa Lindi na kubainisha kuwa Kilwa ilikuwa na wagonjwa 53, Lindi Manispaa (48), Nachingwea (14) na Ruangwa (4).

"Hadi kufikia tarehe 15 mwezi huu wa Julai, wagonjwa tuliokuwanao katika vituo vyetu ni 105, idadi ambayo inaendelea kupungua," alisema Dk. Kagya.

Mkurugenzi Mfaume, akizungumza na watumishi wa idara ya afya katika majumuisho ya ziara yake, alipongeza jitihada zilizochukuliwa kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu bila kuleta vifo vingi kwa wananchi.

Alisisitiza watumishi hao wa afya kuhakikisha tatizo la ugonjwa huo linatoweka na wagonjwa waliobaki vituoni wanahudumiwa na kuwa salama, ili warejea majumbani mwao kuendelea na majukumu ya uzalishaji mali katika maeneo yao.

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ASMAA KHAMSWAN KIMARO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT NO, TAE 279223 ILIYOTOLEWA NA OFISI YA UHAMIAJI 13 JAN 2000 DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA: PHQ/ KIL/MOS/16539/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**FELISIANA SABAS CHAMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye jina la umiliki **KUKU NZITO LTD,** lenye usajili namba **T 634 BPK, CHASSIS NAMBA: 97SF10766 na ENGINE NAMBA: 10766.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/KIL/MOS/16635/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GASTON MELTUS FRANCIS** naomba kutangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE160235 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu tarehe 06/08/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/143813/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**SAID JUMANNE MYOMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye kadi namba: **7528187** na usajili namba **T 809 BZN.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/SIN/MAN/5450/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**DICKSON RICHARD SHIRIMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 669 CWH** na **CHASSIS NAMBA: MD2A21BXXMML86888**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/3945/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HEZRON JACKSON EXAVEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0965/0195/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **USHIROMBO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.


**POLISI TAARIFA: PHQ/KAG/BUK/9214/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.25/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU FRANK VICTOR wa NKUHUNGU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ISABELLAH F. MAPUNDA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi 07 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 04 Mwezi 07 Mwaka 2024.



## Wagombea vijana TLS kupambana na vishoka

**Na Pilly Kigome**

WAGOMBEA nafasi ya urais na uenyekiti, mawakili vijana kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), wamejinadi kurudisha chama hicho kuwa na nguvu ya awali kwa kutimiza misingi halali ya uchaguzi na kuondokana na vishoka katika taaluma hiyo.

Baadhi ya wagombea wa nafasi ya urais TLS, walisema hayo walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya ofisi hizo jijini Dar es Salaam baada ya kumalizika kwa mdahalo uliowakutanisha wagombea hao.

Wakili Revocatus Kuuli, alisema kuna baadhi ya watu wanakiona chama hicho kupoteza ubora, lakini wagombea ambao tunagombea sasa tumeweka mikakati ya kukirudisha chama kuwa na nguvu na kutekeleza misingi iliyojiwekea chama.

Alisema chama kikipoteza misingi na kukosa watu makini, lazima kitayumba na dhamira ya wagombea wajao ni kukirudisha kiwe katika misingi imara.

Naye Wakili Sweetbert Nkuba, alisema kama atapata dhamana ya kukiongoza chama hicho atahakikisha atasambaratisha vishoka walioko kwenye taaluma hiyo ambao hawajasomea sheria.

Alifafanua atahakikisha mawakili wote wanasajiliwa katika chama ili kugundua wababaishaji kwa kutaka kutambua waliposajiliwa, ofisi zao zitambulike kisheria ili kuwabaini wale wababaishaji wasio na ofisi wazuiwe wasifanye kazi za uwakili.

"Kuna baadhi ya watu wanaojiita mawakili wanafanyia kazi zao za uwakili hata baa, sasa hao mimi nikipata dhamana tutacheza nao kwa maana wanaharibu taaluma," alisema.

Alisema kuimarisha TLS kunatakiwa kuwe na sauti moja ambayo kitaimarisha chama na ikiwamo na kupatikana viongozi wenye umakini na dhamira thabiti ya kusimamisha chama na si ujanja ujanja.

Aidha, alisema akipata dhamana atahakikisha anasaidia mawakili vijana chipukizi wasitozwe ada nyingi kuwa mawakili, kuwajengea weledi kwa kuwa mawakili wengi wanashindwa kutekeleza kazi zao kwa kukosa mitaji na maeneo ya kufanyia kazi.

"Nitahakikisha kupatikana kwa maslahi ya mawakili, bima ya afya na bima ya maisha kwa mawakili, vituo vya malezi kwa mawakili vijana pamoja na kuboresha mahusiano na kuunganisha mawakili na taasisi muhimu za serikali ikiwamo mahakama na jamii," alifafanua.

Naye mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa mawakili vijana, wakili Denis Bwana alisema kwa kupitia Sheria namba 307 ya Bunge katika kifungu cha nne, TLS ina wajibu kuishauri serikali, kuishauri Bunge TLS kuwa ni chombo cha mfano katika jamii kwa kusaidia masuala ya kisheria nchini.

# Hali bado tete baada ya hitilafu ya kiteknolojia

**AUSTIN,** Texas

BIASHARA na huduma kote duniani bado zinashuhudia hitilafu, huku zingine zikianza kurejea polepole baada ya hitilafu kubwa ya teknolojia kuathiri mifumo ya kompyuta siku ya Alhamisi na Ijumaa.

Ilielezwa kuwa biashara za benki, hospitali na mashirika ya usafiri ya ndege zilikuwa miongoni mwa zile zilizoathirika pakubwa baada ya kampuni ya usalama mtandaoni 'CrowdStrike' kutelekeza programu mpya iliyokuwa na hitilafu na ambayo iliathiri programu zinazotumia 'Microsoft Windows'.

Mkuu wa Kampuni ya CrowdStrike aliomba msamaha kwa hitilafu hiyo na kusema kwamba imerekebishwa, huku akikiri kwamba itachukua muda kabla ya programu zote kufanya kazi vizuri bila matatizo.

Ikiwa baadhi ya huduma za mashirika ya ndege zikitarajiwa kurejea utoaji huduma kama kawaida baada ya maelfu ya safari kusitishwa, mashirika hayo yalisema huenda changamoto za kucheleweshwa na kufutwa kwa safari zikaendelea kushuhudiwa kwa siku za usoni.

Pia ilibainishwa kwamba biashara nyingi sasa ziko mbioni kutimiza maagizo ya wateja na huenda hatua hiyo ikachukua siku kadhaa.

Huduma za afya nchini Uingereza, Israel na Ujerumani pia zilikumbwa na matatizo, na baadhi ya huduma zilisimamishwa.

Hitilafu hiyo iliyoshuhudiwa duniani kote ilizua wasiwasi kuhusu mfumo na udhibiti wa mtandao wa teknolojia duniani kote, na jinsi hitilafu katika mfumo mmoja inaweza kuwa na athari kubwa kiasi hicho katika sekta mbalimbali.

Ilibainishwa kuwa tatizo lenyewe lilianza Alhamisi saa 1:00 usiku likiathiri watumiaji wa programu ya Windows inayotumia mfumo wa usalama mtandaoni wa 'CrowdStrike Falcon'. Lakini kwa mujibu wa Microsoft, ukubwa wa tatizo lenyewe ulidhihirika Ijumaa asubuhi.

Ilielezwa kuwa hadi kufikia Ijumaa jioni, changamoto hiyo ilikuwa imeshughulikiwa katika sehemu nyingi duniani, huku viwanja vingi vya ndege vikisema kwamba kulikuwa na matatizo katika mifumo ya malipo ya wateja.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa wakati tatizo hilo likitokea safari nyingi za ndege zilikuwa zimeanza. Na hadi sasa huduma zimerejea kuwa kawaida katika uwanja wa ndege wa Hong Kong, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya China.

Vile vile, wakati hayo yakijiri, benki kubwa zaidi nchini Marekani ya JP Morgan Chase, ilisema iko mbioni kurejesha huduma za mashine za fedha za (ATM). **BBC**



Jeshi la Polisi nchini Bangladesh likifanya doria baada ya kupiga marufuku ya kutotoka nje kwa wananchi ili kukomesha maandamano. **PICHA: MTANDAO**

## Wananchi 115 wauawa maandamano Bangladesh

**DHAKA,** Bangladesh

WANAFUNZI nchini Bangladesh wameongoza maandamano yakilenga kupinga mfumo wa serikali wa kugawa ajira wanaosema ni wa kibaguzi, hali iliyosababisha kuweko kwa makabiliano makali na polisi na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 115 hadi jana.

Kutokana na hali hiyo serikali nchini humo jana ilitoa amri ya watu kutotoka nje, ikiwa ni moja ya hatua za kukabiliana na sintofahamu hiyo.

Ilielezwa kuwa wanajeshi walionekana wakifanya doria kwenye miji mbalimbali nchini humo, kujaribu kuzuia maandamano ya wanafunzi hao.

Maandamano yanayoendelea yanaelezwa kuwa changamoto kubwa kwa Waziri Mkuu Sheikh Hasina ambaye amekuwa madarakani kwa miaka 15, huku jeshi likitumwa kusaidia kuleta utulivu, kwa mujibu wa msemaji wa jeshi Shahdat Hossain.

Msemaji huyo wa jeshi alisema watu hawataruhusiwa kutembea mpaka saa nne asubuhi, huku jiji kuu Dhaka likidhibitiwa vikali hali iliyowalazimu wakazi karibu wote kusalia ndani ya nyumba zao.

Aidha, ilielezwa kuwa maandamano hayo yalianza kushuhudiwa Ijumaa, na kusababisha makabiliano kati ya waandamanaji na polisi wanaodaiwa kutumia nguvu kupita kiasi hali iliyosababisha watu150 kulazwa hospitali wakiwa na majeraha ya risasi. **RFI**

## DRC yasitisha uchimbaji madini Kivu Kusini

**KIVU,** DRC

MAMLAKA ya Mkoa wa Kivu Kusini nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), imesitisha shughuli zote za uchimbaji madini katika eneo hilo ikielezwa kuwa hatua hiyo imefikiwa ili kurejesha utulivu katika sekta hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na mamlaka ya Kivu, kuanzia leo Julai 22, maeneo yote ya uchimbaji madini yatakuwa hayafanyi tena kazi, ikiwa ni agizo la gavana mpya wa mkoa huo, Jean Purusi, ambaye aliteuliwa na kuanza kazi tangu mwezi Juni.

Alisema shughuli zitasitishwa kwa jumla katika maeneo yote katika mkoa huo wenye utajiri wa dhahabu, cassiterite, coltan na malighafi nyinginezo, madini yanayochimbwa hasa kwa njia ya ufundi na makampuni chini ya sheria za Kongo, lakini yenye mitaji ya kigeni, hasa ya Kichina. **RFI**

## HABARI MICHEZO

# AZAM YATUMA SALAMU NGAO YA JAMII IKIPIGA 3-0 MOROCCO

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC, kimetuma salamu kuelekea mechi za Ngao ya Jamii zitakazoanza Agosti 8, mwaka huu baada ya kupata ushindi wake wa kwanza katika mechi za kirafiki dhidi ya US Yacoub Al Mansour ya nchini Morocco juzi usiku.

Azam FC imepata ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya kujipima nguvu dhidi ya timu hiyo ya daraja la tatu katika mchezo uliochezwa saa 2:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, ikiwa ni moja kati ya mechi tatu ambazo itacheza ikiwa Morocco.

**Ilifunga mabao yake yote kipindi cha kwanza kupitia kwa Cheikh Sidibe, Gibril Sillah na Jhonier Alfonso Blanco.**

Kocha Youssouph Dabo, ameonyesha kufurahishwa na ushindi huo, ingawa alisema bado anaendelea kukisuka kikosi kwani hakijakamilika kwa asilimia zote ambazo wao kama benchi la ufundi wanahitaji.

“Tunaendelea kukisuka kikosi na kwa bahati nzuri ni kwamba mazingira ya kambi huku ni mazuri sana, kuanzia viwanja, kumbi za mazoezi ya gym, pamoja na vyakula, hivyo nategemea baada ya muda mfupi tu kikosi kitakuwa imara zaidi.

“Tuna mechi tatu huku za kujipima nguvu kabla ya kurejea, moja tayari, kwa hiyo baada siku chache tutacheza nyingine na tutakapomaliza ya tatu, kikosi kitakuwa kimekamilika, tutarejea nchini tayari kwa mashindano yanayotukabili,” alisema.

Azam itacheza mechi yake ya Ngao ya Jamii dhidi ya Coastal Union, Uwanja wa New Amaan, Zanzibar, Agosti 8, saa 10:00 jioni, na mshindi wa mchezo huo atakwenda kucheza fainali Agosti 11, mwaka huu na mshindi kati ya Simba na Yanga, mchezo utakaopigwa siku hiyo hiyo, saa 1:00 usiku, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## MAZOEZI...



Vijana wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa kituo hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kuogelea Taifa matumaini makubwa Olimpiki*

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Timu ya Taifa ya Kuogelea Tanzania, limesema halina wasiwasi na waogeleaji wao, Sophia Latiff na Collins Saliboko, wanaojiandaa kuelekea Paris nchini Ufaransa hapo kesho kwenda kuchuana kwenye mashindano ya Olimpiki yatakayoanza Julai 26, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mkurugenzi wa Ufundi wa Chama cha Mchezo wa Kuogelea Tanzania (TSA), Amina Mfaume, alisema kutokana na maandalizi waliyowapa, anaamini watakwenda kuipeperusha vema bendera ya Taifa.

“Kwa upande wetu tumewaandaa vizuri kisaikolojia waogeleaji wetu ili wakienda huko waweze kufanya vizuri kwa kupunguza muda wao na kurudi na medali za ushindi,” alisema Mfaume.

Mkurugenzi huyo alisema wamekuwa wakishiriki mashindano mbalimbali ambayo yamewasaidia kuimarisha zaidi viwango vyao.

Alisema wanaendelea kuzungumza nao kwa lengo la kuwaondoa hofu pindi watakapokutana na waogeleaji wengine kutoka mataifa mbalimbali, kwa kujiamini ili watimize malengo yao.

Kwa upande wa mchezaji, Saliboko, ambaye ni mara yake ya kwanza kwenda kuchuana kwenye mashindano hayo makubwa duniani, alisema yuko tayari kushindana kutokana na mazoezi waliyoyafanya kwa kipindi kifupi.

“Tulianza kufanya maandalizi mapema kupitia mashindano mbalimbali ya kimataifa tuliyoshiriki ambayo yametufanya tukidhi vigezo vya kwenda Olimpiki,” alisema Saliboko.

Alisema malengo yake ni kwenda kuvunja rekodi za waogeleaji waliopita huku pia akiishukuru Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), kutokana na ushirikiano waliowapa.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi, alisema kwa sasa wanafanya mazoezi ya mwisho ili kuimarisha pumzi zao.

## JKU kuiwindia Pyramids Dar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU SC inatarajia kuweka Kambi Tanzania Bara kujiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo wataikaribisha Pyramids ya Misri, Agosti 17, mwaka huu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa JKU, Shazil Khatibu, alisema kambi yao hiyo wanatarajiwa kuweka katika viunga vya Mbweni JKT.

Alisema wanatarajia kuanza kambi hiyo Agosti Mosi mpaka watakapoikaribia mechi hiyo.

“Sisi uongozi tunaendelea na maandalizi yetu ya kuhakikisha timu inapatiwa kile mwalimu anakihitaji hasa katika kuelekea mchezo wetu huu muhimu,” alisema.

Aidha, alisema kupitia michuano ya Kagame ambayo timu hiyo imeshiriki wameona kikosi chao ambacho kilikuwa na maingizo mapya mengi kinaweza kufanya vizuri ikiwa kitapata muda wa maandalizi.

## Washiriki 1,000 kuchuana vikali Marathon Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya washiriki 1,000 wa mbio za marathon kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, wanatarajiwa kuchuana vikali jijini Arusha kuanzia Desemba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa wakati wa hafla ya uzinduzi wa mbio hizo, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko wa Kampuni ya Tanfoam, Gloria Temu, alisema mbio hizo zitafanyika katika kanda tatu na awali wataanza na ufunguzi Kanda ya Kaskazini.

“Makao makuu ya mbio ni Arusha, lakini zitaongezeka kwenda kwenye mikoa mingine kwa mzunguko wa mikoa mitatu iliyoko kanda tatu nchini, ambayo ni Dodoma na Mwanza,” alisema Gloria.

Alisema lengo kuu la mbio hizo ni kuelimisha jamii kutambua umuhimu wa kufanya mazoezi na kula vizuri ili kuboresha afya zao kwenye utendaji wa kazi.

Glori alisema kutakuwapo na mbio za nusu marathon (kilomita 21), mbio za kilomita 10 na mbio za kilomita tano ambazo zitakuwa zinawahusu washiriki wanaopenda mazoezi mepesi wakiwamo watoto na wazee.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MOUNT KUPIGWA BEI**

KLABU ya Manchester United ipo tayari kumuuza kiungo wa kati wa Uingereza, Mason Mount mwenye umri wa miaka 25, msimu huu wa joto. ***(HITC)***

**RABIOT KUTUA UNITED**

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kusaini Manchester United baada ya kuondoka Juventus mwishoni mwa mkataba wake. ***(Mail)***

**SETFORD ATAKIWA ARSENAL**

ARSENAL inajiandaa kumsajili mlinda mlango wa Uingereza, Tommy Setford mwenye umri wa miaka 18, kutoka Ajax kabla ya ziara yao ya kwenda Marekani. ***(Evening Standard)***

**LINDSTROM MKOPO EVERTON**

KIUNGO wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kucheza kwa mkopo wa msimu mzima pale Everton kutoka Napoli. ***(CalcioMercato)***

**KANTE KUTUA WEST HAM**

KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mdomo ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante, 33, kutoka Al Ittihad. ***(The Athletic)***

**GOMEZ AWINDWA**

KLABU ya Brighton imefanya mazungumzo na Inter Miami kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Paraguay, Diego Gomez, 21. ***(Sky Sports)***

**AWANIWA BIRMINGHAM**

KLABU ya Birmingham City imeelekeza macho yao kwa kiungo wa Fulham na Wales, Luke Harris, 19. ***(Football Insider)***

**VILLA KUMUUZA DIGNE**

ASTON Villa inajiandaa kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Lucas Digne, 31. ***(Football Insider)***

**UGARTE SAFI UNITED**

KIUNGO wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte, 23, amekubaliana maslahi binafsi na Manchester United, ambao wanaendelea kufanya mazungumzo na Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano)***

**MCTOMINAY AWEKEWA BEI**

MANCHESTER United imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

**ALVAREZ ATAKIWA PSG**

KLABU ya Manchester City itafanya mazungumzo na mchezaji wao wa kimataifa wa Argentina, Julian Alvarez, 24, baada ya Copa America. PSG wanavutiwa na mshambuliaji huyo ambaye anataka muda zaidi wa kucheza, lakini City wanataka kusalia naye. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAMNASA BEKI MAHIRI ITALIA EURO 2024

**LONDON,** England

ARSENAL imefikia makubaliano na Bologna kwa ajili ya kumsajili Riccardo Calafiori, kwa mujibu wa ripoti.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alifurahia msimu mzuri katika ngazi ya klabu, akiisaidia Bologna kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini ni uchezaji wake akiwa Italia kwenye Euro 2024 ulikuwa wa kuvutia zaidi.**

Thamani ya Muitaliano huyo imepanda sana kwa sababu ya uchezaji wake, na kuhakikisha Bologna itapata faida kubwa - licha ya klabu ya zamani ya Basel kuwa na kipengele cha kupata asilimia 50 katika dau la pauni milioni 3.4.

**Tayari Calafiori amekubaliana na maslahi binafsi ya mkataba wa miaka...**

Mazungumzo na Arsenal - klabu itakayoibuka mbele ya foleni ya kutaka kumsajili Calafiori - kuhusu dili la euro milioni 50 yalikuwa yakiendelea kwa wiki kadhaa, huku pande zote mbili zikitafuta kujadili muundo wa malipo unaokidhi mahitaji yao.

Bologna ilisemekana kutaka dau la euro milioni 45 pamoja na euro milioni 5 katika nyongeza, ikijumuisha malipo ya juu - kitu ambacho Arsenal walitaka kukipunguza na kuweka vifungu vya ziada na vivutio vya siku zijazo.

The Athletic kwanza iliripoti kwamba Arsenal 'wanaharakisha' juhudi zao za kumsajili Calafiori na walitaka kukamilisha dili la beki huyo mahiri 'haraka iwezekanavyo', wakijua kwamba klabu nyingine zinamfuatilia.

Fabrizio Romano sasa amefichua kuwa makubaliano yamefikiwa, ambayo yatawafanya Arsenal kulipa ada ya uhakika ya euro milioni 40 katika nyongeza na inajumuisha kifungu cha mauzo.

Calafiori, ambaye aliombwa kuhudhuria mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya na Bologna huku dili likiendelea, tayari amekubaliana maslahi binafsi ya mkataba wa miaka mitano.

HABARI MICHEZO

# KOCHA ATOA ONYO USAJILI WA WILLIAMS

**LONDON,** England

KOCHA wa Athletic Club, Ernesto Valverde, amewaonya wanaomwania winga, Nico Williams, kwamba haamini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, anataka kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto.

Williams alicheza vema katika rada za uhamisho za wachezaji mashuhuri wa Ulaya msimu uliopita na akainua hisa zake kwa kiwango kipya na jukumu zuri katika kikosi cha Hispania kwenye Euro 2024.

Arsenal, Chelsea na Barcelona zote zinamwania mchezaji huyo mwenye asili ya Ghana. Winga huyo kwa sasa yuko likizo baada ya uchezaji wake msimu huu wa majira ya joto na Valverde amesisitiza Athletic wanasubiri kwa hamu kurejea kwake.

"Sina shaka na Nico," alisema Valverde akiviambia vyombo vya habari. "

"Anaonekana mzuri na mwenye furaha. Mwaka huu tuna changamoto nyingi mbele yetu na nina uhakika Nico atapenda kukabiliana nazo.

"Hakuwa mchezaji pekee ambaye amelazimika kuishi na tetesi kwa sababu soko litakuwa wazi hadi mwishoni mwa Agosti. Ni mchezaji mzuri na kunaweza kuwa na klabu ambazo zinaweza kumtaka, lakini anafurahi nasi na tunafurahi naye. Tunamtegemea Nico atakaporudi kutoka likizo.

"Tunatamani kuwa na wachezaji bora na kwamba anataka kuwa nasi. Tuna mwaka ambao tumeufurahia sana. Tuna timu nzuri sana na kama tunaweza kuiboresha, tutafanya hivyo."

Kuna kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa Williams cha euro milioni 58 ambacho kinawakilisha thamani ya ajabu katika soko la usajili, inaeleka kuwa Chelsea tayari imeonesha wasiwasi juu ya mahitaji ya juu ya mshahara wa winga huyo.

Inasemekana kuwa anapokea kiasi cha euro 200,000 kwa wiki na Chelsea wanasitasita kwenda juu sana. Ripoti zinaonyesha kuwa Williams anapendelea kujiunga na Barcelona, ambapo wachezaji wenzake wa kimataifa wa Hispania wamemtaka hadharani kumhitaji kucheza naye.

Lamine Yamal hajaficha hamu yake ya kucheza pamoja na rafiki yake wa karibu katika ngazi ya klabu na kiungo Pedri hivi majuzi alituma ujumbe kwa Williams.

"Atakuwa na usajili mzuri kwa Barca," alisema Pedri akiambia The Residency.

"Katika Euro, sote tuliona kile anachoweza kufanya."

Williams anaripotiwa kuwa amepewa hadi Agosti 12, mwaka huu kupumzika baada ya Euro 2024 na anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake kabla ya kurejea.




## Chelsea kumalizana na Lukaku

**LONDON,** England

CHELSEA na Napoli zinafanya mazungumzo juu ya uhamisho wa kudumu wa Romelu Lukaku, kwa mujibu wa ripoti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alijiunga tena na Chelsea katika msimu wa majira ya joto wa 2021 kwa ada ya rekodi ya klabu ya pauni milioni 97.5, lakini haraka hakuwa na wakati mzuri baada ya mwaka wa kwanza mgumu huko Stamford Bridge.

Lukaku alisaini mkataba wa miaka mitano aliporejea Chelsea, akiwa amecheza nafasi kubwa katika ushindi wa Inter wa taji la Serie A msimu wa 2020/21, na mshahara wake mkubwa umemzuia kuondoka kwa msingi wa kudumu licha ya kuwa wazi kuwa hana mustakabali huko magharibi mwa London.

Inter ilimchukua Lukaku kwa mkopo msimu wa 2022/23 na Roma walifanya vivyo hivyo msimu uliopita - muda ambao alifunga mabao 23 katika mechi 57 za Serie A. Sky Sports imeripoti kwamba uhamisho wa muda mrefu wa kuhamia Napoli, ambao utamkutanisha Lukaku na kocha wake wa zamani Antonio Conte, sasa uko kwenye mstari, huku pande hizo mbili zikijadili muundo wa uhamisho wa kudumu.

Mbelgiji huyo tayari amekubaliana na Napoli na ana nia ya kufanya kazi na Conte kwa mara nyingine.

Mkataba unaweza hatimaye kuwezesha kuondoka Victor Osimhen - lengo la muda mrefu la Chelsea, lakini pia kipaumbele cha kwanza kwa miamba ya Ligue 1, Paris Saint-Germain.

# *Ten Hag: Sasa ni muda wa Sancho kung'ara*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amemtaka Jadon Sancho "kujiimarisha zaidi" baada ya kurejea katika klabu hiyo kutokana na mgogoro wa hadharani kati ya wawili hao msimu uliopita.

Sancho aliichezea Man United kwa mara ya kwanza tangu Agosti mwaka jana katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Rangers, juzi Jumamosi.

Alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund, na kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kumkosoa hadharani Ten Hag katika chapisho lake la mtandao wa kijamii.

Lakini baada ya kufanya mazungumzo na Ten Hag mapema mwezi huu, Sancho amerejea mazoezini na kikosi cha kwanza.

"Tulizungumza vizuri," alisema Ten Hag akiiambia AD Sportwereld ya Uholanzi kabla ya ushindi wa mabao 2-0 ya mchezo wa kirafiki Jumamosi.

"Kila mtu anaweza kufanya makosa. Ikiwa mchezaji atatafakari hili vizuri, wewe chora mstari na kusonga mbele.

"Klabu hii inahitaji wachezaji wazuri, na jambo moja ni hakika: Jadon Sancho ni mchezaji mzuri sana. Natumai kwamba bado atafanya vizuri na kwamba atachangia mafanikio yetu."

Licha ya uvumi mkubwa juu ya mustakabali wake, Ten Hag alisaini mkataba mpya kubaki hapo Man United msimu huu wa majira ya joto.

Kocha huyo wa zamani wa Ajax alichukua mikoba hiyo Old Trafford mnamo 2022 kutoka kwa bosi wa muda Ralf Ragnick ambaye alidai timu hiyo inatakiwa kufanya jambo la ziada ili kurudia utukufu wake wa zamani.

"Rangnick alikuwa sahihi kabisa," Ten Hag aliongeza kwa AD Sportwereld. "Tumekuwa tukifanya kazi kwa bidii juu ya hili kwa miaka miwili, lakini alisema ni sawa kabisa ni operesheni ya kina, ngumu sana. Na nilijua nilipoanza kuwa itakuwa kazi ngumu."

Muundo uliopo karibu na Ten Hag umebadilika sana katika miezi ya hivi karibuni kutokana na kuwasili kwa Sir Jim Ratcliffe kama mmiliki mpya.

Ten Hag alielezea dalili za awali za kufanya kazi pamoja na Mkurugenzi wa Michezo mpya, Dan Ashworth, Mkurugenzi wa Ufundi, Jason Wilcox na Mkurugenzi wa Uajiri, Christopher Vivell kama "nzuri sana."

Tayari msimu huu wa majira ya joto, United imemsajili beki chipukizi Mfaransa Leny Yoro kwa ada ya awali ya Euro milioni 62, pamoja na fowadi wa Uholanzi, Joshua Zirkzee kwa zaidi ya Euro milioni 40 kutoka Bologna.

Klabu hiyo pia inaendelea kuvutiwa na walinzi Matthijs de Ligt wa Bayern Munich na Jarrad Branthwaite wa Everton, vyanzo vimeiambia ESPN.

"Sitatoa maoni mahususi iwapo tutavutia majina hayo mawili au la," alisema Ten Hag.

HABARI MICHEZO

## Kocha Augsburg aichambua Yanga

INATOKA UK. 24

Mabao ya washindi yalifungwa na beki wa kushoto raia wa Dermark, Mads Pedersen, dakika ya 37, na winga wa kushoto Mjapan Masaya Okugawa, akapachika bao la pili dakika ya 80, huku straika Mkongomani Jean Baleke, akifunga bao la kufutia machozi dakika nne kabla ya mechi kumalizika baada ya kuunganisha kwa kichwa krosi iliyochongwa na Mkongomani mwenzie, Maxi Nzengeli.

Yanga itaingia tena dimbani Jumatano kucheza dhidi ya TS Galaxy na Jumapili Julai 28, itamaliza mechi zake nchi humo kwa kucheza dhidi ya Kaizer Chiefs, mechi ya Kombe la Toyota, kwenye Uwanja wa Bloemfontein.

## Mutale atabiriwa makubwa Simba

INATOKA UK. 24

yake na staili anayopenda kucheza na anataka kikosi chake kicheze kwa kasi sana, hivyo anahitaji wawe na pumzi ya kutosha.

"Nadhani 'pre season' inakaribia kumalizika, wiki iliyopita tulicheza mechi ya wenyewe kwa wenyewe, yaani wachezaji wangu niliwagawanya na kukipiga, nimeona jinsi wanavyopambana, ushindani ulikuwa mkubwa sana, ila tunataka kubalansi baadhi ya maeneo machache tu, lakini kikubwa ni kwamba zaidi ya asilimia 90 kila kitu kiko sawa, eneo la ufiti wa wachezaji tumelifanyia kazi kwa kiasi kikubwa kwa sababu soka langu nataka wachezaji wacheze kwa spidi sana, hivyo ni lazima wawe na pumzi ya kutosha na utimamu wa mwili, kilichopo sasa ni kutafuta muunganiko, sasa ni wajibu wao uwanja kukimbia kwenye maeneo ya kutengeneza nafasi," alisema.

Alisema anadhani kuna vitu vichache tu vilivyobaki ikiwamo kuwatengeneza wachezaji hasa wapya waweze kujiweka sawa kisaikolojia kucheza mechi ya Simba Day mbele ya mashabiki zaidi ya 60,000, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Nawatengeneza wachezaji hasa wapya kwa ajili ya kucheza kwenye uwanja mkubwa kama wa Mkapa, ukiwa na watazamaji 60,000 ili kuweza kuzuia presha pamoja na hisia zao, pamoja na zile watakazozipata kutoka kwa mashabiki," alisema.

Simba inateremka dimbani leo kucheza na timu ya Daraja la Pili nchini Misri, El-Qanah, itakayopigwa saa 11:30 jioni kwa za Tanzania, huku kocha Fadlu, akisema baada ya hiyo kutakuwa na mechi zingine mbili za kujipima nguvu.

# SERIKALI KUKUSANYA BILIONI 200/- MICHEZO KUBASHIRI

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya Sh. bilioni 200 zinatarajiwa kukusanywa kupitia michezo ya kubashiri ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2024, imeelezwa.

**Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya kubashiri nichini (GBT), James Mbalwe, wakati wa uzinduzi wa Kampuni mpya ya Michezo ya Kubashiri ya Betwinner, jijini Dar es Salaam jana.**

Mbalwe alisema kiwango hicho cha fedha ni ongezeko la Sh. bilioni 30 kulinganishwa na makusanyo ya mwaka jana ambayo yalikusanya jumla ya Sh. bilioni 170.

Alisema kuwa sekta ya Michezo ya Kubashi (Sports Betting), kwa sasa inakuwa kiasi cha kuchangia katika mfuko wa taifa na kukuza uchumi wa nchi.

"Sekta ya 'Sports Betting', imepata maendeleo makubwa na kuwa na mchango mkubwa katika kuchangia mfuko wa taifa. Hivyo ujio wa Kampuni ya Betwinner, itaungana na kampuni nyingine kuchangia mfuko wa taifa.

Natoa wito kwa makampuni kuwa waadilifu, kuwa na welidi na uwazi katika kufanya shughuli zake ili kujipatia wateja na kuendelea kukua," alisema Mbalwe. Alisema ujio wa kampuni hiyo utaleta chachu ya maendeleo ya michezo hiyo hapa nchini mbali ya kuleta ushindani.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Shirikisho la Kampuni za Michezo ya kubashiri Tanzania (TSBA), Sabrina Msuya aliipongeza kampuni hiyo kwa kuingia katika soko la Tanzania.

"Nawapongeza kwa kuingia katika soko la Tanzania na kuendeleza sekta hii ambayo kwa sasa inakuwa kwa kasi," alisema Msuya.

Naye Mkurugenzi wa Masoko wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Aaron Nyanda alitoa wito kwa kampuni hiyo kusaidia ligi zao mbalimbali ikiwa pamoja na Championship na nyinginezo.

Pia aliipa angalizo kampuni hiyo kutotumia katika matangazo picha za wachezaji ambao hawana haki nazo ili kuepuka kuingia katika kesi ambazo zimetokea tayari na kampuni nyingine kushindwa.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa Betwinner, Jesse Ndambala, alisema wanafuraha kubwa kuingia nchini na kuchangia pato la taifa huku wakiwa na malengo mengine mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidia maendeleo ya michezo na jamii.

Ndambala alisema ujio wao umelenga kuwapa wateja 'odds' nzuri zaidi tofauti na kampuni nyingine za kubashiri. Alisisitiza kuwa wameleta ubunifu mkubwa katika michezo yao ya kubashiri ikiwa ni pamoja na kuwapa asilimia 100 ya bonasi kwa wateja wapya ikiwa ni sehemu ya ofa ya ukaribisho.

"Mbali na kuwa na odds nzuri, tumeweka ubunifu mkubwa katika michezo yetu na kutoa asilimia 100 ya bonasi kwa wateja wapya. Lengo hapa ni kuongeza burudani na chachu ya ushindani kwenye sekta ya michezo.

"Mbali na soka, pia tutaangalia jinsi gani ya kuwekeza katika michezo mbalimbali kama gofu, netiboli na mingineyo, " alisema Ndambala.



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini Ismailia nchini Misri walipoweka kambi kujiandaa na msimu mpya. **PICHA: SIMBA**

## *Timu za Majeshi zatakiwa kupigania michuano CAF*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU za Majeshi zimetakiwa kufanya usajili mzuri wa wachezaji ili ziweze kushiriki mashindano ya kimataifa kama zinavyofanya Simba, Yanga pamoja na Azam FC.

Hayo yalisemwa juzi jioni na Meja Jenerali Maiko Jocob Muhona, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, kwenye ufunguzi wa mashindano ya Mkuu wa Majeshi (CDF Cup 2024), yanayoendelea kwenye viwanja mbalimbali Dar es Salaam.

"Tunatamani kuona timu za majeshi zinashika nafasi za juu na kupata fursa ya kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa kama zilivyo Simba Yanga na Azam FC," alisema.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kuazimisha Miaka 60 ya Jeshi la Ulinzi na kudai yatasaidia kuunda timu itakayoshiriki katika mashindano ya timu za Majeshi (Bamata) Septemba, mwaka huu, mkoani Morogoro.

Aidha, alimpongeza Mkuu wa Majeshi kwa kuamua kuyarudisha baada ya kutofanyika kwa kipindi cha miaka miatano, na kuwataka waamuzi watendeke haki katika michezo yao ili kuepusha malalamiko ya hapa na pale.

Pia aliwataka vijana washiriki michezo kwani inajenga afya pamoja na kuwasaidia kupata ajira kwa urahisi.

Wakati huo huo, Brigedia Jenerali Said Hamis Saidi, alisema mashindano hayo yameshirikisha Kamandi mbalimbali za jeshi ikiwamo nchi kavu, majini, anga pamoja na ile ya akiba.

"Kutakuwa na michezo mbalimbali itakayoshirikisha wanaume na wanawake ukiwamo mpira wa miguu riadha netiboli na kulenga shabaha , alisema Jenerali Saidi.

Vile vile alisema mwaka huu wameongeza mchezo wa ngumi na kurusha mpito wakiwa na malengo ya kupata wachezaji watakaokidhi vigezo vya kwenda kushiriki mashindano ya Olimpiki ifikapo mwaka 2028 nchini Marekani.

Michezo

Jumatatu Julai 22, 2024

Nipashe



Arsenal yamnasa Calafiori UKURASA 21

NJOONI...



Beki wa Kulia wa Yanga, Yao Kouassi, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Augsburg FC, kwenye mechi ya Kombe la Mpumalanga, iliopigwa Uwanja wa Mbombela, Afrika Kusini juzi na Wajerumani hao kushinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# KOCHA WA AUGSBURG AICHAMBUA YANGA

**Adam Fungamwango na**

**Shufaa Lyimo**

## ●●● Aikubali huku Gamondi akisema bado hapo anatesti mitambo tu kwani...

WAKATI Kocha Mkuu wa Augsburg, Jess Thorup, inayocheza Ligi Kuu ya Ujerumani Bundlesliga, akiimwagia sifa Yanga kutokana na kiwango ilichoonyesha katika mechi ya juzi nchini Afrika Kusini, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema bado anaendelea kutengeneza kikosi kwani ana muda mfupi tu tangu aanze maandalizi, lakini akiridhishwa na vijana wake.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi maalum ya kuwania Kombe la Mpumalanga, ukichezwa Uwanja wa Mbombela, nchini humo na Yanga kupoteza kwa mabao 2-1, Gamondi alisema pamoja na kikosi chake kuwa na siku chache tu tangu kianze maandalizi, lakini ameridhishwa na kiwango hasa kipindi cha pili.

**"Kwetu tumeupokea vizuri huu mchezo kwa sababu usisahau tumecheza na timu ya kiwango cha juu sana, hii timu huwa inacheza dhidi ya Bayern Munich, Leverkusen na Dortmund, kwetu sisi ndio kwanza tunaanza maandalizi na nimeona tumekuwa tunapoteza mipira kirahisi, lakini ni kawaida kwa hatua hii ya maandalizi," alisema Gamondi.**

Alisema ameridhishwa na viwango vya wachezaji wake kwani katika muda huu ambao wanarejea kutoka majumbani wakati mwingine baadhi wanakuwa hawapo vizuri.

"Kwa ujumla nimeridhishwa na viwango vya wachezaji wangu, kipindi cha kwanza wapinzani wetu walipoteza nafasi kama tatu hivi, sisi tulipoteza mbili, kipindi cha pili tulitawala na kutengeneza nafasi ambazo tungeweza kusawazisha hata dakika za mwisho," alisema raia huyo wa Argentina.

Naye kocha wa Augsburg ambayo msimu uliomalizika ilikamata nafasi ya 11 katika Ligi Kuu ya Ujerumani, Thorup, aliimwagia pongeza Yanga, akisema ina wachezaji wenye nguvu, wanaocheza soka la kasi, lakini baadhi wakiwa na vipaji binafsi.

"Yanga ni timu nzuri, ina wachezaji wenye nguvu, baadhi wana vipaji binafsi, wana kasi na wanacheza kwa kasi sana na hata bao lao la kufutia machozi lilikuwa bora sana.

"Nashukuru tulimiliki mpira dakika 45 za kwanza, kipindi cha pili kwangu hakikuwa kizuri hatukuweza kumiliki kama cha kwanza, Yanga wakimiliki mchezo kipindi hicho," alisema kocha huyo.

INAENDELEA UKURASA 23

# Mutale atabiriwa makubwa Simba

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza, Kikosi cha Simba ambacho kina idadi kubwa ya wachezaji wapya, kinatarajiwa kushuka leo kwenye Uwanja wa Old Suez Canal, kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya El-Qanah ya nchini humo, huku Kocha Mkuu, Fadlu Davis, akimtabiria winga, Joshua Mutale, kuwa mmoja wa wachezaji watakaong'ara sana ndani ya kikosi chake msimu ujao.

Akizungumza akiwa Ismailia nchini Misri ambako kikosi hicho kinajiandaa na msimu mpya wa mashindano, Fadlu alisema katika mazoezi ya timu hiyo, moja ya kitu anachoshuhudia ni kipaji na uwezo mkubwa wa Mutale katika kutafuta nafasi yeye mwenyewe, kuwatengeneza wenzake, lakini akiwa hatari zaidi anapobaki na beki mmoja.



Kocha huyo mpya raia wa Afrika Kusini, alikuwa akizungumzia maendeleo ya maandalizi ya kikosi chake, huku akisema yanaelekea ukingoni.

"Hapa tuna Mutale, yeye ana uwezo mkubwa mno na kukimbia kwenye nafasi, kutengeneza nafasi kwa wenzake, ni hatari anapobaki na beki mmoja, nadhani anaweza kung'ara sana kwenye kikosi chetu, kingine tunachoangalia ni kutengeneza safu ngumu ya ulinzi na jinsi ya kucheza wakati hatuna mpira, na hapa naangalia kipaji cha mchezaji mmoja mmoja, nini anafanya wakati ana mpira na anachotoa wakati timu haina mpira mguuni. Kikosi cha Simba lazima kicheze kwa staili ya kuvutia," alisema kocha huyo.

Alikuwa akizungumzia aina

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >